Nipashe
Ijumaa Agosti 30, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581784
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US


Bilionea Afrika Kusini ampiku Dangote kuongoza utajiri Afrika
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Uwekezaji pamoja na unavyotunisha mifuko kwa usalama, kuanzia mtaji Sh.10,000
USUKANI WA UCHUMI UNAVYOSHIKWA...
Samia anavyoendesha 'SU'; mwongozo wa Mzee Mwinyi, ubunifu na mahitaji ya leo

**Biteko**: Tanzania tuko tayari kwa uzalishaji nyuklia UKURASA 3

**Kaka** amng'ang'ania mdogo wake kortini madai kumdhulumu milioni 860/- za zabuni ya barabara UK. 3

**Waliokamatwa** kwa amri ya DC, wafunguliwa kesi uhujumu uchumi UKURASA 8

UKURASA 11

SHERIA MPYA MAFAO

# Mlolongo ahueni kwa mchangiaji

UKURASA 2



- Rukhsa kuchangiwa na waajiri wawili
- Mchango wako kukopea benki
- Idadi kuongezwa wanufaika kifamilia
- Mazuri kwa wastaafu wanaorudi kazini
- Wenye ulemavu waandaliwa mazuri

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana, Ajira, na wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete akiwasilisha muswada wa sheria ya marekebisho ya Sheria za Hifadhi za Jamii wa Mwaka 2024, bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia Suluhu Hassan akimtunuku nishani ya miaka 60 ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF) Jenerali Jacob Mkunda, kwenye hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Jacob, Malisa waomba korti iwaachie huru

UK. 5



## Wabunge waibana serikali hali mbaya vileo 'visungura'

UK. 5

**MICHEZO** SIMBA YAFUNGUKA, DABO HANA PRESHA UK.24

**MAONI,** UK.6



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbosa (kushoto) akifafanua jambo kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuf Mwenda (katikati), alipotembelea Bandari ya Tanga, mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mlolongo ahueni kwa mchangiaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 wenye mlolongo wa mambo kadhaa yenye ahueni kwa mchangiaji.

Katika muswada huo, waajiri wamepunguziwa adhabu ya kuchelewa kuwasilisha michango na kutoa rukhsa kwa mfanyakazi aliyeajiriwa na mwajiri zaidi ya mmoja kuchangiwa na wote kwa ridhaa yake.

Vilevile, mwanachama ambaye hajafikia umri wa kustaafu, ameruhusiwa kutumia sehemu ya mafao yake kama dhamana kwa mkopo wa nyumba huku watu waliojiajiri wenyewe katika sekta binafsi wakiruhusiwa kujiunga na kunufaika na mafao ya hifadhi ya jamii katika mpango wa uchangiaji kwa mujibu wa sheria.

Muswada huo pia umeruhusu michango iliyowekwa na mwanachama baada ya umri wa kustaafu hadi kufikia miaka 70 kuzingatiwa katika ukokotoaji malipo ya mafao ya pensheni.

Akiwasilisha muswada huo bungeni jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, alisema marekebisho hayo yanagusa sheria tatu ambazo ni Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50; Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371; na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263.

Waziri huyo alisema kimeongezwa kifungu cha 11A kinacholenga kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii kwa watu waliojiajiri.

Pia alisema muswada huo umeruhusu mwajiri kuchangia kwa kiasi kikubwa au kiasi chote na Kifungu cha 12(5) kimependekezwa kurekebishwa kuainisha namna ya uchangiaji kwa wanachama waliojiajiri.

"Kifungu cha 12A kimeongezwa ili kuruhusu mfanyakazi aliyeajiriwa na mwajiri zaidi ya mmoja kuchangiwa na waajiri wote kwa ridhaa yake. Lengo la marekebisho haya ni kumpa mwanachama uhuru wa kuchangiwa na zaidi ya mwajiri mmoja," alisema.

**PUNGUZO LA ADHABU**

Ridhiwani alisema kifungu cha 14(3) kimerekebishwa ili kupunguza adhabu ya tozo kutoka asilimia tano (5) hadi asilimia mbili na nusu (2.5) inayotozwa na mfuko kwa mwajiri kwa kuchelewa kuwasilisha michango ya mfanyakazi na lengo ni kuainisha kiasi stahiki cha faini na kupunguza gharama za uendeshaji kwa waajiri na kuweka tozo rafiki na zinazolipika.

Ridhiwani alisema wameongeza makosa mapya kwa mwajiri anayekataa kujiandikisha na mtu yeyote anayemzuia mkaguzi wakati wa kutekeleza majukumu yake, kuwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka au ofisa wa mfuko aliyeteuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua kesi yoyote ya jinai chini ya sheria.

Waziri huyo alisema muswada huo umependekeza kumwezesha Mkurugenzi Mkuu kuteua jopo la madaktari ili kuthibitisha iwapo mwanachama amepata ulemavu wa kudumu na lengo la ni kuhakikisha mafao yanatolewa kwa mnufaika anayestahili.

Pia alisema muswada umeongeza kiwango kinacholipwa kwa wategemezi pale ambapo mwanachama atakuwa amefariki dunia kutoka miezi 33 hadi 36.

Alisema muswada umeweka masharti ya lazima kwamba waajiriwa wa kampuni ambayo serikali inamiliki angalau asilimia 30 ya hisa, ni lazima wasajiliwe kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Alisema pia muswada huo unaboresha masharti yanayohusiana na kumbukumbu za michango ya mwajiriwa pindi itakapohitajika ili kumwezesha mwanachama kupata historia ya uchangiaji wake kwenye mfuko.

"Kifungu cha 24 kimefutwa ili kuondokana na dhana iliyojengwa katika kifungu hicho inayoruhusu mwanachama kutoa kiasi cha mchango wake katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kuondolewa uanachama, inakinzana na Kanuni za Hifadhi ya Jamii kutokana na dhana ya kifungu hicho kutumiwa kwenye Mfuko wa Akiba na si katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii," alisema.

**WALIO GEREZANI**

Ridhiwani alisema masharti yamewekwa mnufaika wa mafao ambaye kwa kipindi husika anatumikia kifungo, anaweza kuridhia kwa maandishi kwamba mafao yake au sehemu yoyote ya mafao yake ilipwe kwa mnufaika atakayetajwa.

"Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ushiriki wa mtu anayetumikia kifungo katika utoaji mafao yake kwa mnufaika," alisema.

Waziri huyo alisema kifungu cha 48(6) kinapendekezwa kurekebishwa ili kumwezesha mwajiriwa ambaye amepata ulemavu wa kudumu kuendelea kupokea pensheni hata baada ya kurejea kazini au kupokea mafao ya uzeeni.

## Sakata la utekaji, kupotea watu laibuka Bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SAKATA la matukio ya utekaji, mauaji na kupotea watu limeibuliwa tena bungeni huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwaomba wananchi kusaidia vyombo vya ulinzi na usalama ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wahusika wa mambo hayo.

Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni katika kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Anatropia Theonest. Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali wa kuzuia vitendo hivyo,.

"Kuna matukio yanaashiria uvunjifu wa amani. Matukio haya ni utekaji, mauaji na upoteaji wa watoto na yamekuwa na sura tofauti ikiwamo wivu wa kimapenzi lakini pia ushirikina na matukio mengine ya kutekwa na kuuawa watu yanayohusisha vyombo vya dola," alisema mbunge huyo.

Hata hivyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kabla ya kumpa nafasi Majaliwa kujibu swali hilo, alisema juzi alisimama Mbunge wa Nkasi, Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, akizungumzia suala hilo na kwamba mambo hayo yanahitaji uchunguzi.

"Ukiyasema kwa ujumla haya maneno ya utekaji, mauaji, leo asubuhi nimesoma kuna mganga amezika watu zaidi ya 10 sasa wale ni vyombo vya dola?"

"Kila mwanadamu ana haki ya kuishi. Msiweke mazingira ya kuonesha kwamba kila anayepotea ni vyombo vya dola, kuna watoto, kuna mabasi wanapanda kule chini akidondoka njiani familia ikimtafuta utasema ni chombo cha dola kimemchukua? Wakati wote tunabidi tufanye hii kazi kama viongozi. Tukitumia mihemko hatutoi nafasi kwa serikali kufanya kazi yake wakati huo huo hatutoi nafasi kwa jamii kuendelea kushiriki hili jambo.

"Waziri Mkuu labda utoe maelezo ya jumla kuhusu hilo lakini kuhusu swali sisi wote humu ndani ni viongozi na tunawakilisha wananchi tungependa wananchi wawe salama. Sasa ukisema mambo ya jumla jumla chukua nafasi kama kiongozi unaweza kushauri lakini usinyoshe vidole kwa kuwa huna uhakika,"alisema Spika.

Akijibu swali hilo, Waziri Mkuu alisema wanapolinda nchi ni wajibu wa Watanzania wote kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

"Tunavyo vyombo vya ulinzi na usalama vyenye jukumu la kupokea taarifa mbalimbali zilizoonesha uvunjifu wa amani popote pale na jukumu lao wakishapokea taarifa ni kuhakikisha wanafanya uchunguzi. Uchunguzi utakapobaini waliotenda makosa wanachukuliwa hatua kwa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Alisisitiza kuwa, serikali imeendelea kusimamia misingi na kudhibiti mambo yanayotishia amani ya nchi na usalama wa raia na mali zao.

"Suala la ulinzi na usalama bado liko mikononi mwetu pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Jukumu letu ni kusaidia vyombo vya ulinzi kwa kutoa taarifa taarifa zozote zile zinazoleta tishio la amani katika nchi ili vyombo vyetu vichukue tahadhari na hatua stahiki ili kuwabaini wale wote wanaosababisha kutokuwapo kwa amani katika nchi yetu,"alisema.

Majaliwa alimshukuru Spika kwa maelezo yake ya awali ili kuondoa upotoshaji unaoendelea kufanywa na kusababisha vyombo kushindwa kufanya kazi na kuwavunja moyo watu wanaofanya kazi ya ulinzi saa 24 ili kuhakikisha nchi inabaki salama.

## HABARI KITAIFA

# Makalla atoa miezi 10 ujenzi wa hospitali ukamilike

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Halmashauri Kuu ya Taifa ( NEC) ya Chama Cha Mapinduzi, Amos Makalla ametoa muda wa miezi 10 kwa mkandarasi anayejenga Hospitali ya Mbagala Rangitatu, kuhakikisha anakamilisha ujenzi ili ianze kutoa huduma na kupunguza adha kwa wananchi.

Pia amemwagiza kuweka miundombinu wezeshi hospitalini huko kwa watu wenye ulemavu na wazee watakaokuwa wanafika kupata matibabu.

Alitoa maagizo hayo jana huko Mbagala, Dar es Salaam alipokagua ujenzi wa hospitali hiyo yenye ghorofa sita unaogharimu Sh. bilioni 10.

"Ninakuagiza mkandarasi (Group Six International Ltd) ifikapo Juni mwakani, ujenzi wa hospitali hii uwe umekamilika kwa sababu Oktoba mwakani tuna jambo letu.

"Hatutaki kumwangusha Rais Samia Suluhu Hassan ambaye serikali yake imeshatoa fedha nyingi za ujenzi wa hospitali na vituo vya afya," alisema Makalla.

Alisema anafahamua kuhusu ujenzi wa hospitali hiyo kwa kuwa akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alishiriki kuanzia hatua ya kwanza hadi Akitoa maelezo kuhusu sekta ya afya wilayani Temeke, Mganga Mkuu wa Manispaa ya Temeke, Dk.Jonas Lulandala alisema wilaya ina vituo vya afya 179. Kati yake, vya umma ni 30, binafsi 133, dini 17 na taasisi za serikali viwili.

Alisema Hospitali ya Mbagala ina uwezo wa kuhudumia wananchi 438,141, wajawazito 130 na wanaofanyiwa operesheni (saba).

Dk. Lulandala alisema hospitali hiyo ina watumishi 235 wenye ajira za kudumu na wa mkataba 55.

Dk. Lulandala alisema hospitali mpya itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kulazwa wagonjwa 165, kutoa huduma za kibingwa ikiwamo kufanya operesheni kwa wagonjwa saba hadi 14 kwa siku.

Alisema pia itakuwa na wodi za watoto, wanaume na wanawake pamoja na kutoa huduma za kujifungua kwa kinamama 30 hadi 40 kwa siku.

Mbunge wa Mbagala, Abdallah Chaurembo alisema: "Tunashukuru serikali kwa kutupatia Sh. bilioni mbili za kuanza ujenzi wa hospitali hii."




Mkuu wa Mawasiliano wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Tanzania, Catherine Mbatia (mwenye mkoba), akipata maelezo kutoka kwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian, Mikocheni Viwandani, Dar es Salaam jana. Wengine ni Naibu Meneja Mkuu wa TGL, Jackson Paulo (kulia), Meneja wa Fedha wa kampuni hiyo, Samwel Orgeness (wa tatu kulia), Ofisa Mawasiliano wa EACOP Tanzania, Abass Abraham (wa pili kushoto), Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Epson Luhwago (kushoto) na Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Matangazo ya TGL, Eliupendo Lema. **PICHA: JOHN BADI**

# Aliyeombwa kumsamehe mdogo wake mil. 800/- atafuta haki mahakamani

**Na Moses Ng'wat,** MBEYA

NDUGU wawili wa damu wamefikishana katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya huku kaka mtu akimshtaki mdogo wake kwa tuhuma za kuchepusha Sh. 860,127,540.

Katika shauri hilo la madai namba 19 la mwaka 2022, Nawabu Abdullahman ambaye ni kaka na Mkurugenzi wa kampuni ya Batallion Construction Limited ya mkoani Tabora, amedai mahakamani kuwa fedha hizo zilitokana na malipo ya mradi wa matengenezo ya barabara waliyotekeleza kwa ubia na kampuni ya Jalal ya Jijini Mbeya katika barabara ya Chang'ombe hadi Patamela, wilayani Songwe.

Alidai kuwa kampuni yake na mbia zilimteua mdogo wake, Faheed Abdullahama, kuwa msimamizi wa mradi huo uliotekelezwa kati ya mwaka 2018 na 2021. Pamoja na kuteuliwa kufanya kazi hiyo, bila uhalali wa kisheria alichepusha fedha hizo na kuingia kwenye akaunti yake binafsi ya benki baada ya serikalini, kupitia Wakala wa BarabaraTanzania (TANROADS) Mkoa wa Songwe kufanya malipo.

Mleta maombi (mdai) huyo aliiambia mahakama kuwa mdogo wake ambaye wamechangia baba, kutoka kwa mama tofauti, baada ya kugundua kuwa amechepusha fedha hizo, alipeleka malalamiko yake mbele ya familia.

Alidai kuwa baada ya familia, akiwamo baba yao mzazi kupokea na kufanya usuluhishi, aliombwa kusamehe kwa kuwa Mungu angemlipa jambo alilodai kutoridhika nalo na kuamua kukimbilia mahakamani ili kutafuta haki zaidi.

Mleta maombi huyo aliiomba mahakama hiyo kutazama kwa kina ushahidi na madai yake hayo ili kupata haki yake, ikiwemo kupewa fidia mahususi (special demage) kwa kuwa mdogo wake mbali na kuchepusha fedha zote za malipo, aliondoka na kuitelekeza kampuni na kazi za mradi zilizosalia hali iliyoilazimu kampuni kuingia gharama za ziada kumalizia mradi.

Shahidi wa upande wa mdaiwa (wajibu maombi), Fahid Abdullahman (30), alidai kuwa hajawahi kutelekeza kazi za mradi kama ilivyodaiwa na mleta maombi, bali Mkurugenzi wa kampuni ya Batallion Construction Limited ambaye ni kaka yake ndiye aliamua kumwondoa kwenye usimamizi wa mradi huo.

Pia alidai kuwa alikuwa na haki ya kupata asilimia 50 kwa kuwa yeye ni sehemu ya mbia na kwamba alikuwa anadai madai zaidi ya Sh. Milioni 600 na kwamba baada ya kutolipwa alipeleka madai hayo kwa familia kwa usuluhishi lakini haikufanikiwa.

Alidai kuwa aliondolewa kazini baada ya kaka yake kutaka kumdhulumu fedha zake baada ya kukusanya mapato lakini hakumpatia asilimia 50 ya mapato kama makubaliano yalivyofanyika kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Akihojiwa na wakili wa mleta maombi, Hassan Kilingo, Fahid alikiri kwamba January 15, 2021 alipokea Sh. milioni 200 kutoka kampuni ya Btallion, huku akikana kupokea kiasi kingine cha Sh. million 23 kwa kuwa kwenye nyaraka haikuonekana.

Katika kesi ya msingi, Nawabu anaomba kurejeshwa kwa fedha hizo ili utaratibu wa kugawana ufanyike kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba, ikiwaemo kulipwa fidia mahususi.

# Biteko aeleza utayari Tanzania matumizi nyuklia

**Na Mwandishi Wetu,**
NAIROBI

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko ameeleza mpango na utayari wake wa nchi katika uendelezaji wa nishati ya nyuklia ikiwa ni moja ya vyanzo mbadala vya nishati safi ya umeme kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

Dk. Biteko ambaye pia ni Waziri wa Nishati, aliyasema hayo wakati akiwasilisha Mpango wa Tanzania katika mkutano wa pili wa masuala ya Nishati ya Nyuklia kati ya Marekani na nchi za Afrika (US-Africa Nuclear Energy Summit) unaoendelea jijini Nairobi, nchini Kenya.

Mkutano huo unajumuisha viongozi katika sekta ya nishati, watunga sera na wataalam kutoka nchi mbalimbali barani Afrika.

Dk. Biteko alisema Tanzania iko tayari kuendeleza nishati ya nyuklia ikiwa ni moja ya vyanzo vitakavyoiwezesha nchi kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika na ambao unakidhi viwango vya kimataifa katika uhifadhi wa mazingira.

"Utayari wa Tanzania katika kuendeleza na kutumia nishati ya nyuklia unatiliwa mkazo katika sera ya nishati ya mwaka 2015, sera ya madini ya mwaka 2009, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme na Mkakati wa Nishati Jadidifu ambapo nyaraka zote hizi zinatambua umuhimu wa nyuklia kukidhi mahitaji ya nishati nchini," alisema.

Aidha, alisema chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, serikali inaendelea kuchukua hatua muhimu zitakazowezesha matumizi ya nishati nyuklia kama moja ya vyanzo vya nishati safi ambapo hadi sasa Tanzania ina mashapo ya madini ya urani takriban tani 58,500 ambayo yanaweza kutumika kama chanzo cha uzalishaji wa nishati ya nyuklia.

Alifafanua kuwa, uwapo wa vyanzo mbadala vya umeme utawezesha nchi kuboresha ushirikiano wake kibiashara na nchi nyingine ndani na nje ya Bara la Afrika na kuboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Mpango huu wa kuwa na umeme wa kutosha utawezesha hatua ya kuunganisha gridi za umeme miongoni mwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika na baadaye katika maeneo mengine ya bara hili," alisema Dk. Biteko.

Alisema nia ya Tanzania ni kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo nchi ya Marekani na Bara la Afrika, ili kuendeleza nishati ya nyuklia hasa ikizingatiwa kuwa takriban watu milioni 600 barani Afrika na biashara ndogondogo zipatazo milioni 10 bado zinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Kwa mujibu wa Dk. Biteko, mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanakua kwa asilimia 10 hadi 15 kwa mwaka na ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Tanzania imepanga kuzalisha megawati 10,000 za umeme ifikapo mwaka 2030.

Msaidizi Maalum wa Rais wa Marekani wa Masuala ya Uhifadhi wa Mazingira, Fedha na Uvumbuzi, Nana Ayensu, alisema mkutano huo ni muhimu kwa nchi washiriki katika kufungua milango ya uendelezaji wa nishati ya nyuklia ambayo ni rafiki kwa matumizi ya binadamu na hifadhi ya mazingira na pia kuimarisha ushirikiano miongoni mwa nchi husika.

Aliongeza kuwa nishati ya nyuklia itafanikisha ajenda za kimataifa za nishati safi zinazoendelea, ikiwamo nishati safi ya kupikia inayopigiwa chapuo kimataifa huku kinara wake akiwa ni Rais Samia.

Kuhusu utayari wa nchi yake, alisema Marekani ipo tayari kushirikiana na nchi za Afrika ili kuendeleza matumizi ya nishati ya nyuklia ambayo inatoa uhakika wa upatikanaji nishati na kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

IITA Transforming African Agriculture CGIAR IRRI

**POSITION ANNOUNCEMENT**
**Administrative and Finance Assistant**
**IITA-TZ-2024 - IRRI-010 -NRS- DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Rice Research Institute (IRRI) invites applications for the position of **Administrative and Finance Assistant**

**Background:** The International Rice Research Institute (IRRI) is a nonprofit independent research and training organization. IRRI is a member of the Consultative Group of International Agricultural research (CGIAR) Consortium.

Under the supervision of the **Senior Admin Assistant - Administrative Coordination, the Administrative and finance Assistant** will provide overall day to day secretarial and administrative support to the Senior admin assistant - Administrative Coordination and to all unit.

Responsible for the daily activities needed to run the IRRI cash offices. Process all cash transactions accurately and efficiently in accordance with established policies and procedures.

**Duty Station:** The position will be based in IITA Mikocheni offices in Dar es Salaam.
Qualifications and experience
- Bachelor Degree in Business Administration with minimum 1 year of relevant work experience.

**Skills and knowledge**
**mandatory**
- Knowledge of MS Office (Word, Excel, PowerPoint)
- Good oral and written communication skills, communicates status of work regularly and in a timely manner
- Must be scrupulously honest and always foster an atmosphere of trust and integrity.
- Ability to perform fast, efficient and maintain discretion and confidentiality
- Have basic knowledge of accounting.

**Preferred**
- Good interpersonal skills and Good organizational skills

**Responsibilities**
**1.1. Purpose**
- Preparing and posting expenses reports on OCS, preparing bank reconciliation each month from Tanzania Bank accounts and Counterchecking receipts
- Manage filing and distributing all incoming and outgoing mail/faxes/letters/documents.
- Receive incoming mail and invoices and direct them to the appropriate services.
- Assist with staff and visitors travel arrangements and bookings for flights, accommodation and local transport as requested
- Tag assets and make reconciliation
- Photocopy and scan documents
- Keep track of basic office supplies by maintaining inventory and assist to order new/additional basic office supplies as needed.
- Assist in the application and processing of import and export permits for research and other materials.
- Process cash advance requests
- Reporting discrepancies s/he finds within the accounts to his/her supervisor
- Ensure Compliance with expenditure commitment procedures

**1.2. Engagement**
- Efficient and effective administrative support for staff and visitors
- Ensuring all programs and operations have adequate support needed
- Reporting discrepancies s/he find within the accounts to his/her supervisor
- Compliance with expenditure commitment procedures

**1.3. Delivery**
- Improve efficiency and dealing with a diverse group of callers and visitors at all levels, both internal and external to IRRI, and ensure all are treated in a professional and courteous manner.
- Cash reconciliation reports
- Advance register well maintained

**General information:**
The duration of the contract is two years renewable subject to performance and availability of funds. These are nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

The application pack should include an application letter, copies of certificates, and a curriculum vitae which contains a telephone number, email address, and contact details of two referees. Applications should be sent by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org** and addressed to:

The Country Representative, IITA-Tanzania,
Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road,
Mikocheni Industrial Area,
Dar es Salaam, Tanzania

Applicants are requested to include the r**eference number for the position** (as indicated on the heading of the announcement) in the subject of their application letter, as well as in the subject of their email. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date for applications: Friday 13th September 2024.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# TGNP yapendekeza mambo 6 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025-2050

**Na Halfani Chusi,**
KONDOA

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), Umependekeza Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo itakayoanza mwaka 2025-2050 izingatie mambo yanayogusa jamii ikiwamo kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Mambo mengine yaliyopendekeza ni kuondoa vifo vitokanavyo na uzazi, kulinda usalama wa chakula, upatikanaji wa maji, umeme, pamoja na kuifanya Tanzania kuwa jumuishi katika makundi yote.

Hayo yalisemwa jana wilayani Kondoa mkoani Dodoma na Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa Mtandao huo, Zainabu Mmari katika tamasha la siku tatu la saba la jinsia ngazi ya wilaya kwa mwaka 2024.

Zainabu alisema mtandao huo katika uchambuzi wake ulibaini Dira ya Maendeleo 2025 inayotamatika, wananchi wengi hawakushirikishwa katika mchakato wa kutoa maoni na pia hawakuielewa wakati wa utekelezaji wake.

"Bado kuna ombwe kubwa la kijinsia ambalo limejitokeza katika maeneo matano yaliyowekwa kama vipaumbele vya dira.

"Changamoto tuliyoiona au ombwe lililokuwapo ni kwamba wananchi walikuwa hawana uelewa kwamba hiki tunachokifanya ndicho kinaenda kutekeleza dira kufikia yale maisha bora tuliyoambiwa. Hivyo, mwisho wa siku tulikuwa tunatekeleza bila kuelewa tunafanya nini ili kufikia malengo yaliyofikiwa," alisema.

Alisema katika tamasha hilo wameangalia pia kwa kiasi gani makundi yote katika jamii hususani wanawake na wale wanaoishi pembezoni walipata fursa ya kushirikishwa katika mchakato wa dira.

Alisema licha ya mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika maeneo kadhaa, kuna ombwe kubwa la kijinsia ambalo limejitokeza katika maeneo matano ambayo yaliwekwa kama vipaumbele vya dira akitoa mfano maeneo ya kijinsia hayakupewa kipaumbele kikubwa.

Aliseme changamoto nyingine waliyoibaini ni kutokuwapo kwa viashiria vya kupima hii dira hasa kwenye masuala ya jinsia.

Alisema kutokana na changamoto hiyo ndio sababu kubwa iliyofanya TGNP kuendelea kuweka mkazo na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutoa maoni katika dira ijayo. 0755629279

"Mpaka sasa tumeelimisha wananchi wengi sana kuelewa dira inayomalizika, lakini pia kuweka maoni yao kwenye dira ijayo kuhakikisha kuwa maoni yao yanachukuliwa ili kuwa na Tanzania wanayoitaka katika miaka 25 inayokuja katika dira ya mwaka 2025- 2050," alisema Zainabu.

Mratibu wa vituo vya taarifa na maarifa kutoka Kata ya Ukenyenge, Kishapu Mkoa wa Shinyanya, Fredina Saidi, alisema namna walivyoshirikishwa utoaji wa maoni kwenye dira umejenga ufahamu mkubwa kwa wanajamii.

Alisema kupitia ushirikishwaji uliofanywa na TGNP wameweza kuelewa ni namna gani wanaweza wakatoa maoni hususani kwa mambo ambayo yanawahusu katika upande wa afya, maji, elimu miundombinu pamoja na usalama nchini.

"Sisi kama jamii tuna jukumu kubwa la kuangalia matatizo na mapungufu yetu ambayo tunayo ndiyo tuweze kutoa maoni kuhusu mambo gani tunatamani yawe," alisema.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Fatma Nyangasa, alitaka wakazi wa wilaya hiyo kuitumia vyema elimu waliyoipata kupitia tamasha hilo.

Alisema tamasha hilo lenye dira isemayo 'Dira Jumuishi ya 2050, miaka 30 Beijing tujipange' ni tamasha lenye umuhimu na lenye tija kwa taifa kwa sababu yote yanayoibuliwa yatafanyiwa kazi na kuleta tija.

# Sababu lishe duni Morogoro zaanikwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

ULAJI usiofaa wa vyakula na mila potofu ni miongoni mwa sababu zinazofanya Mkoa wa Morogoro kuwa na hali duni ya lishe licha ya kuwa moja ya mikoa inayozalisha chakula kwa wingi nchini.

Akitoa taarifa katika kikao cha Tathmini ya Utekelezaji wa Mkataba wa Lishe, Ofisa Lishe wa Mkoa wa Morogoro, Salome Magembe, alisema mambo hayo ndiyo sababu kubwa na kwamba sasa ufike wakati wananchi kuondokana na mila hizo na kuzingatia ulaji mzuri wa vyakula.

"Licha kwamba wakazi wa mkoa huu wengi wao wanazalisha mboga nyingi za majani na matunda ya aina mbalimbali kila msimu , bado jamii nyingi hazitumii vyakula hivyo kama sehemu ya mlo wa kila siku." alisema.

Magembe alisema hali halisi ya lishe ya mkoa wa Morogoro pamoja na kiwango cha udumavu kwa watoto walio chini ya miaka mitano ni asilimia 30.6.

Pia, alisema kiwango cha uzito pungufu kwa watoto walio chini ya miaka mitano kimefikia asilimia 3.9 huku upungufu wa damu kwa watoto chini ya miaka mitano ukiwa asilimia 68.1.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe kwa kila robo ya mwaka wa fedha.

Alisema wapo wakurugenzi watendaji wa Halmashauri za Mkoa huo hutoa fedha hizo wakati wa robo ya mwisho wa mwaka, hali inayozorotesha utekelezaji wa mkataba huo.

Malima aliwaagiza wakurugenzi hao, kila mmoja kutoa Sh. 1,555 kwa kila mtoto aliye chini ya miaka mitano ndani ya halmashauri yake kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa afua za lishe.

Katika hatua nyingine, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwenye utekelezaji wake wa afua za lishe kwa mwaka wa fedha 2023/24, ilitenga Sh milioni 76. 8 .

Meya wa Manispaa hiyo , Pascal Kihanga, alisema hivi karibuni katika hotuba yake ya taarifa ya utendaji na uwajibikaji wa manispaa hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwenye mkutano wa mwaka wa baraza la madiwani .

## Jacob, Malisa waomba mahakama iwaache huru

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Meya wa Ubungo Dar es Salaam, Boniface Jacob na Godlisten Malisa, wameiomba mahakama itumie kifungu namba 226 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (CPA), kuwaachia huru kama upande wa Jamhuri wakishindwa kuleta shahidi Oktoba 3, 2024.

Katika kesi hiyo washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matatu likiwamo la kusambaza taarifa za uongo mtandaoni kwa lengo la kupotosha umma kuhusiana na kijana aliyedaiwa kupotea.

Malalamiko hayo waliyatoa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kupitia wakili wao, Peter Kibatala wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa shahidi wa kwanza wa upande wa Jamhuri.

Kibatala alidai hayo, baada ya Wakili wa Serikali Mwandamizi, Job Mrema kuieleza mahakama kuwa kesi ililetwa kwa ajili ya usikilizwaji na walikuwa na shahidi mmoja aliyefika mapema asubuhi eneo la mahakama.

"Kwa mujibu wa rekodi za mara ya mwisho kesi ilipangwa kusikilizwa, kwa upande wetu tunaomba ahirisho la shauri hili, shahidi aliyefika kwa ajili ya kutotoa ushahidi kabla ya shauri kuitwa alianza kujisikia vibaya."

"Akaomba kwenda kujitazama afya yake, kutokana na sababu hii imesababisha tumeomba ahirisho na hii hali ipo nje ya uwezo wetu sisi mawakili," alidai Wakili Mrema.

Wakili Kibatala alidai kuwa, ni hoja rahisi aliyoitoa Wakili Mrema ya kutaka kesi iahirishwe na kudai kuwa kwa muda huo anayoyasema hayo ni saa sita na robo mchana, na kuhoji kwa nini hawakupewa taarifa hiyo mapema ili waondoke kwenda kwenye majukumu mengine.

"Hoja yao ni rahisi sana, Mheshimiwa hujui hata shahidi ni nani, tunaomba utoe ahirisho la mwisho na tunaomba urekodi kwamba kama ukiridhia ahirisho hili, kama siku itakayopangwa Jamhuri hawataleta shahidi, basi mahakama itawaachiwe huru chini ya Kifungu namba 226 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (CPA) na pia kama itawezeka kesi iahirishwe mwezi mzima kwa sababu nitakuwa na mashauri mengine kama wenzetu hawatakuwa na tatizo," alidai Kibatala

Kibatala aliendelea kudai kuwa, kama itawezekana mahakama ipange Septemba 26, 2024 kwa usikilizwaji.

Akijibu hoja hizo, Wakili Mrema alidai kuwa wapo makini na kesi hiyo na wamefanya kila namna kuhakikisha shahidi kapatikana na katika maelezo ya Kibatala hakuna alipokataa kwamba shahidi hajafika mahakamani.

Pia, alidai kuwa suala la kutokutaja jina la shahidi hawaoni kama inaathiri haki ya upande wa pili, aliomba mahakama ipuuze hoja hiyo kwa sababu suala la ugonjwa haliwezi kuepukika.

Alidai kuwa, kuhusu ahirisho la mwisho na hoja ya kifungu cha 226, hiyo hana cha kueleza kwa sababu mahakama ndiyo inapima na kuhusu tarehe 26 kama itawezekana iende wiki inayofuata. Baada ya kusikiliza hoja hizo, Hakimu Swalo alisema kwa sababu wamesema shahidi alikuwapo ndiyo akajisikia vibaya anakubali ahirisho hilo lakini hakutegemea kuwapo na shahidi mmoja kwa sababu kesi hiyo ina mashahidi wengi.

"Leteni mashahidi wengi kama hawatakuwapo bado mahakama itaona itakachofanya. Hivyo, naahirisha kesi hadi Oktoba 31, 2024 saa nne asubuhi," alisema Hakimu Swalo.

Ilidaiwa kuwa Aprili 22, 2024, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Jacob kwa lengo la kupotosha umma, alisambaza taarifa ya uongo kupitia mfumo wa kompyuta wenye jina la Boniface Jacob @ExmayorUbungo wenye kichwa kilichosomeka 'wenye leseni ya kuua wameua tena'.



Wakili Hekima Mwasipo (kulia) akisalimiana na wateja wake, aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob na Mtetezi wa Haki za Binadamu, Godlisten Malisa (kushoto), kabla ya kuanza kusikiliza kesi inayowakabili ya kuchapisha taarifa za uongo kwenye mitandao ya kijamii katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Serikali yabanwa madhara ya 'visungura' kwa vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameibana serikali kufanya utafiti na kudhibiti pombe kali ambazo ziko chini ya kiwango zinazosababisha madhara mbalimbali ya kiuchumi na kiafya kwa Watanzania hususan vijana.

Katika kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu bungeni jana, Mbunge wa Hai (CCM), Saasisha Mafuwe, alihoji kuhusu mikakati ya serikali katika kudhibiti vileo vikali ambavyo vinaathiri uchumi wa vijana na ujenzi wa uchumi wa taifa.

"Wanalewa sana wakati wa kazi wakati wa mchana na hii ni kutokana na uingizwaji wa vilevi vikali kutoka nje ya nchi na vilevi ambavyo vinapatikana kila mahali, kiasi kwamba kijana anaweza kwenda gengeni akamiminiwa kinywaji kidogo na kulewa kabisa, hivyo kushindwa kuendelea na kazi. Nini kauli ya serikali juu ya udhibiti wa vileo hivi vikali ambavyo vinaathiri uchumi wa vijana na ujenzi wa uchumi wa nchi yetu?" alihoji.

Baada ya kipindi cha maswali na majibu, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, aliomba mwongozo kwa Spika na kueleza kuwa vijana wanapata madhara ya figo, ini na baadhi ya wanafunzi wa sekondari wanaonunua pombe hizo, wanapata matatizo ya kuona.

Alisema madhara hayo yanasababisha mzigo mkubwa kwa serikali wa kusafisha figo na waathirika wanadhoofika na kushindwa kuanzisha familia.

"Baadhi ya hizi pombe ambazo zinauzwa Sh. 2,000. Kuna zaidi ya aina 10 za pombe kali. Naomba mwongozo wako kwa nini serikali isifanye utafiti wa madhara makubwa yanayowapata Watanzania baada ya kutumia pombe hizo ambazo zipo kwa wingi mtaani.

"Pia kwa nini serikali inaruhusu watu wauze holela wakati kuna leseni zinatakiwa kutolewa kwenye maduka. Ukiona kijana ameshikilia 'energy drink' jua pale hajashikilia 'energy' bali ameweka Shing'waa na pombe hizo ambazo Spika umesema nisizitaje. Kwa nini serikali isifanye utafiti wa pombe hizi zinazoleta madhara makubwa kwa Watanzania," alisema.

Akijibu swali la Mafuwe, Majaliwa alisema serikali ina utaratibu wa kutambua uzalishaji, uuzaji na kudhibiti bidhaa inayoingia nchini ya vileo.

"Vileo hivi vinaendelea kusambaa kwa wateja kwa utaratibu uliowekwa kwa wanaopata vibali vya biashara na kuendesha biashara ya vileo lakini serikali yetu inaendelea kutoa elimu kwa jamii ya kuonesha madhara ya ulevi uliopitiliza. Kama alivyoeleza vijana wengi wanalala wanakosa uwezo wa kufanya kazi," alisema.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kazi kubwa kuhamasisha vijana kujiunga na kutengeneza makundi yenye uwezo wa kufanya shughuli za ujasiriamali na hata mtu mmoja mmoja na kwamba utaratibu huo umesaidia vijana kupata pato linalowezesha kuhudumia jamii zao.

"Tumeona hapa Dodoma pale Machinga Complex, vijana wanafanya shughuli zao. Pia katika wilaya mbalimbali wako vijana wanaendesha bodaboda, bajaji, machinga na wajasiriamali na utaraibu huu umewawezesha kupata kipato," alisema.

Vilevile, alisema serikali itaendelea kutoa elimu kwa jamii kujiingiza kwenye shughuli za ujasiriamali huku wakiimarisha sheria kwa wazalishaji wanaoingiza bidhaa za vilevi nchini, wauzaji na watumiaji hasa wanaokiuka sheria ili kudhibiti kuingia kwa pombe kali kupita kiasi.

"Malengo yetu kila kileo kinachoingia nchini kikidhi kulinda afya za Watanzania, jamii ijiepushe na uingizaji na utengenezaji wa bidhaa zisizo rasmi bila kibali na hawa ndio wanatengeneza bidhaa hizo zenye kileo kupita kiasi," alisema.

Hata hivyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akitoa maelezo ya mwongozo wa Mbunge Matiko, alisema madhara aliyoeleza ni makubwa na yawezekana kuna makubwa zaidi.

"Mbunge amesema anayo orodha ya baadhi ya hizo pombe atakabidhi kwa serikali kufuatilia zinaingia kutoka wapi na kama zinatengenezwa nchini na kujaribu kuona maeneo yale ambayo yameathirika serikali inaweza kuchukua hatua gani," alisema.

Alisema serikali ilichukue jambo hilo na kulifanyia kazi ili kunusuru vijana na watu wengine wasiojua madhara ya matumizi ya pombe hizo na kusababisha idadi ya wanaoumwa magonjwa ya aina hiyo kuongezeka.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Marekebisho Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto ni muhimu

**KUTOKANA** na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyoendelea nchini, Bunge limeelezwa kuwa serikali inatarajia kuleta muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto.

Muswada huo una lengo la kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini.

Suala hili limekuja wakati mwafaka kutokana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kushamiri nchini, hasa kufanyiwa vitendo vya ukatili, utekaji, mauaji na udhalilishaji.

Bunge lilielezwa kusudio hilo la Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, wakati akijibu akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Zodo.

Katika kipindi cha maswali na majibu mbunge huyo alitaka kujua upi mkakati wa serikali kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini hasa kwa wanawake na watoto.

Akijibu swali hilo, Naibu waziri aliliambia Bunge kuwa muswada huo utasomwa katika mkutano huu wa Bunge kwa mara ya kwanza.

Alilifahamisha Bunge kuwa mwezi Mei, mwaka huu serikali ilizindua Mpango Kazi wa Taifa wa awamu ya pili wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II).

Hiyo yote ni katika kuhakikisha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinatokomezwa.

Mikakati mingine iliyotajwa ni elimu kwa umma ambayo imeimarishwa kwa ushirikiano na maofisa polisi ngazi ya kata na kuanzishwa kituo cha huduma kwa wateja wizarani ili kuongeza nguvu ya elimu kwa umma na kupokea taarifa za vitendo vya ukatili.

Huduma za madawati ya jinsia na watoto zimeelezwa kuwa zinapatikana katika vituo vyote vya Jeshi la Polisi pia, idadi ya vituo vya huduma ya dharura na jumuishi kwa manusura wa ukatili imeongezeka na kufikia vituo 26 nchini.

Programu ya elimu ya malezi chanya, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto inatekelezwa kwenye mikoa na halmashauri zote nchini na kwa mwaka wa fedha 2023/24 wizara ilipata kibali cha ajira kwa maofisa Maendeleo ya Jamii 800 na maofisa ustawi 350.

Juhudi hizi za kuanzisha madawati ya jinsia na vituo vya malezi ya watoto, vinasaidia kuripotiwa kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ambayo hapo mwanzo yalikuwa yakiishia kwenye ngazi za familia kwa watu kuogopa kupeleka kwenye vyombo husika kwa hofu ya kutishiwa maisha au kuona fedheha.


Hali hiyo ya kuhofu ndio imesababisha baadhi ya vitendo vya ukatili kuendelea kushamiri na watoto kuteseka kwasababu ya kupata vitisho kwa wale wanao watendea vitendo hivyo.

Utafiti uliofanywa na taasisi mbalimbali umebaini kuwa ukatili dhidi ya watoto mara nyingi hufanywa na watu wa karibu wakiwamo wa ndani ya familia na walio kwenye mazingira yao ya karibu.

Sisi tunasema marekebisho ya sheria ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo hivyo ni muhimu na ikiwezekana hata adhabu zinazotolewa dhidi ya watu wanaofanya vitendo hivyo iongezwe ili visiendelee kufanyika na watoto waishi kwa amani.

Wazazi kwa sasa wanakuwa na hofu watoto wao wanapokuwa nje ya mazingira ya nyumbani kama watarudi salama au kufanyiwa vitendo vyovyote vya ukatili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Mabaya haya yanayosambaa katika jamii, tuhoji mara mbili nafsi zetu

**NI** dhima potofu zimetanda, kuwapa matatizo wengine wakiamini watanufaika kwa kipato kidogo watakapotenda hivyo na wapo wanaotenda mabaya hayo kwa maslahi yao.

Imekuwa tabia sasa watu wanadhuru wengine, katika imani kwamba wanapotenda mauaji na madhara mengine, atanufaika kwa kuuza viungo vya mwili wa binadamu, bila kufikiri kuwa kitendo hicho ni kinyume cha haki za binadamu.

Ni vyema wenye mawazo haya potofu, wakaziyeyusha fikra hizo walizozigandisha, wakiamini mauaji na ukatili unatokea ni njia sahihi ya kuwafikisha uliko utajiri.

Kwa uhalisia, ukweli ni kujikita na shughuli zitakazowanufaisha kama kilimo,ufugaji na ubunifu wa biashara tofauti.

Maisha kanuni yake, hayana njia za mkato kama wengine wanavyodhani, wakatili hao dhidi ya uhai wa wenzao, wanaofanya mauaji ya wengine kuwakata viungo vya mwili, wakiwajumuisha watoto, dada na mama zao.

Tuamke huku tukitanguliza hofu ya Mungu, huku sote wenye taarifa sahihi ya unyama huo tutoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, ambalo liko macho kufanya kazi usiku na mchana kuyakabili hayo.

Jambo la kushangaza ni pale tunasikia na kuona wazazi wengine wanashiriki kuua watoto wao. Tunatakiwa kujua kwamba, hao ni tegemeo la taifa leo na kesho.

Nakumbuka mnamo Juni 18 mwaka huu Jeshi la Polisi lilitangaza kumshikilia baba wa mtoto, pamoja na wenzake kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wa miaka miwili na nusu.

Inatisha na kuumiza kwamba maisha hayana njia ya mkato, kwani zipo shughuli nyingi zinazoweza kuleta maendeleo na kuingiza manufaa halali, daima maisha hufanikishwa kwa kujituma.

Kuna wanaotenda mauaji, kwa sababu ya imani potofu na madai ya 'kuepusha mikosi katika familia au koo zao', pasipo kuangalia upande wa pili mchafu zaidi kusigina haki za binadamu.

Siku zote kwenye jamii, tukiepuka ramli chonganishi zinazoharibu misingi ya familia na ukoo, ndio mwanzo wa madai ya viungo vya mwili wa binadamu.

Ni wakati wa kuamka kutatua matatizo yetu na sio kuyaongeza. Daima mtu anaweza kuingia katika tabu na kupata ukiwa kwa maovu hayo, huku wengine wao wakifanya mauaji, kwa kuamini kuna soko la namna hiyo na wamemeza sumu zinazosababisha ufinyu wa fikra.

Sisi kama jamii jambo hili ni letu sote, hivyo inatupasa kushirikiana na Polisi kuwafichua watu wanaofanya matukio hayo.

Kwani, matukio haya ni chanzo cha kumomonyoka kwa maadili ya vijana na chipukizi, kwa sababu kundi hilo linapokuwa linayaona hayo, wanatamani kuiga, ili waweze kurahisisha maisha.

Nakumbuka simulizi ya kupotea watu nchini Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), imesema inaendelea kufanya chunguzi maalum za matukio hayo kwa lengo la kubaini, pamoja na mambo mengine chanzo na wahusika ili kutoa mapendekezo stahiki.

Ilikuwa Agosti 22, Jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, akawaambia waandishi wa habari kuhusu matukio hayo na kubainisha mikoa inayohusishwa na uchunguzi.

"Uchunguzi huo unaoendelea kwa sasa unahusisha mikoa ifuatayo Dar es Salaam, Singida, Mara, Simiyu,Shinyanga, Mwanza, Kagera, Geita, Kigoma, Tanga, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro, Arusha, Ruvuma na Rukwa.

'Hatua hii ni mwendelezo wa uchunguzi zinazohusu matukio ya kupotea kwa watu ambayo THBUB imekuwa ikiyafanyia kazi katika nyakati tofauti na taarifa zake kufikishwa katika vyombo vinavyohusika," anasema.

Mwaimu anasema kuwa, katika kufanikisha lengo la taarifa iliyotolewa Julai 19, mwaka huu, ikifanyua kazi zilizotekelezwa na THBUB katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, hasa eneo la uchunguzi wa malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji misingi ya utawala bora.

THBUB ilikuwa imekwishafanya hatua mbalimbali ikiwamo uchambuzi wa matukio hayo kwa maana ya sehemu yalikotokea na watu waliokuwa wanadaiwa.

## Mbunge ahoji hatua kulinda theluji ya Mlima Kilimanjaro

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, amehoji serikali imechukua hatua gani za muda mfupi, wa kati na mrefu kunusuru theluji inayotoweka Mlima Kilimanjaro.

Akijibu swali hilo bungeni jijini hapa juzi, Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alisema sababu kubwa ya kupungua kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro ni kuongezeka kwa joto la dunia kutokana na mabadiliko ya tabianchi, yanayochangiwa na ongezeko la shughuli za kibinadamu hususani ukataji wa miti, kilimo, uchomaji moto katika maeneo yanayozunguka mlima, mvua chache na vipindi vya ukame na upepo mkavu kutoka Bahari ya Hindi.

Alisema katika kutekeleza mikakati ya muda mfupi, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanga kupanda miti milioni nane kwa mwaka katika Mkoa wa Kilimanjaro.

"Pia, mikakati mingine ni kutoa elimu kwa umma kuhusu upandaji miti na uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi vya redio, televisheni, matamasha na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa," alisema.

Vilevile, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imezindua kampeni ya kupanda miti zaidi ya bilioni moja katika mikoa ya Kaskazini ili kunusuru barafu ya Mlima Kilimanjaro.

"Mikakati ya muda wa kati ni pamoja na kuhimiza matumizi bora ya ardhi na kuimarisha ulinzi katika maeneo yanayozunguka Mlima Kilimanjaro na kutekeleza mipango ya kudhibiti na kupambana na uchomaji moto mlimani," alisema.

Aidha, alisema katika kutekeleza mikakati ya muda mrefu serikali inaendelea kushirikiana na mashirika ya kikanda na kimataifa kutekeleza mikakati ya pamoja ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kuboresha teknolojia za kilimo, kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji, kupunguza uzalishaji wa gesi chafu na kurejesha mifumo ya ikolojia kwenye mlima na maeneo yanayozunguka.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Salladoo Bakery, Salama Mpanga (kulia), akipokea tuzo ya Mwanamke Mjasiriamali wa Uzalishaji wa Mikate kutoka kwa Mshauri wa Masuala ya Masoko wa Kampuni ya Azam, PriyaRanjan Nath, wakati wa hafla ya usiku wa tuzo kwa waokaji, zilizondaliwa na Umoja wa Waokaji Tanzania (TBA), Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mfamasia Mkuu atoa angalizo usugu wa vimelea dhidi ya dawa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MFAMASIA Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, amewataka wanataaluma wa famasia, wakiwamo wateknolojia dawa, kutoa maelekezo ya matumizi sahihi ya dawa ili kuepusha watumiaji kuwa na usugu wa vimelea dhidi ya dawa ambapo una madhara yanayojumuisha vifo.

Alitoa angalizo hilo juzi mjini Morogoro wakati akimwakilisha Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molel katika hafla ya kufungua mkutano wa mwaka wa Chama cha Wateknolojia Dawa na Wateknolojia Dawa Wasaidizi (TAPHATA) unaofanyika sambamba na kongamano la kisayansi kwa wataalamu hao.

Msasi alisema utafiti wa mwaka 2019 ulibaini kuwa, watu 12,000 walipoteza maisha nchini ndani ya mwaka mmoja kutokana na usugu wa vimelea unaosababishwa na matumizi ya dawa yasiyo sahihi.

Ni hali ambayo Msasi alisema inayoonesha changamoto hiyo inaua idadi kubwa ya watu ukilinganisha na magonjwa mengine.

"Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2018 imebainisha kuwa ifikapo mwaka 2050, zaidi ya watu milioni 10 watafariki dunia kila mwaka kutokana na magonjwa yatokanayo na vimelea ambavyo vimekuwa sugu kutokana na utumiaji usiokuwa sahihi wa dawa," alisema Mfamasia Mkuu wa Serikali.

Kukabiliana na changamoto hiyo, Msasi alisema serikali itaongeza usimamizi wa matumizi sahihi ya dawa ili kupunguza madhara yatokanayo na matumizi yasiyokuwa sahihi ya dawa, hasa aina ya antibayotiki na kuwataka wataalamu wa famasia kuchukua hatua ya mapambano dhidi ya usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa.

"Hakikisheni mnatoa elimu sahihi kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya dawa kwa kuwa ninyi ndio kada ya afya inayohusika zaidi na mnapaswa kulinda afya za wateja wenu," aliagiza.

Pia, ofisa huyo wa serikali aliagiza mamlaka na mabaraza yanayosimamia huduma za dawa na tiba kuhakikisha maduka yote ya dawa yanasajiliwa na kukaguliwa mara kwa mara sambamba na kuhakikisha vituo vyote vya afya vya umma na binafsi vinavyotunza dawa, vinakuwa na mtaalamu stahiki.

"Kuna changamoto pia ya uandikaji dawa kwenye vikaratasi visivyo rasmi ambavyo hata wakati wa kuandikia dawa zinazoingia na kutoka inakuwa changamoto.

"Pia, ufungashaji holela wa dawa mnazotoa, hali inayohatarisha kuwapa matatizo zaidi wagonjwa, mnaweka kwenye bahasha zenye maandishi na zisizo rasmi ambazo wakati mwingine zinakwenda kuharibu dawa," alionya Msasi.

Alielekeza utoaji dawa zote uzingatie mwongozo wa matibabu na orodha ya kitaifa ya dawa muhimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha matumizi sahihi ya cheti cha dawa.

Kuhusu ugonjwa wa homa ya nyani (Mpox), Msasi alisema mpaka sasa hakuna mgonjwa yeyote aliyethibitika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo nchini, hivyo wananchi wasiwe na hofu kwa kuwa nchi iko salama.

Alisema kuwa Agosti 17 mwaka huu, Wizara ya Afya ilitoa taarifa kwa umma kuhusu ugonjwa wa homa ya nyani kutokana na kuongezeka kwa visa duniani, zikiwamo baadhi ya nchi za Afrika Mashariki na hivyo kuujulisha umma kuchukua tahadhari ili kuhakikisha ugonjwa huo haungii nchini.

Aliwataka wataalamu wa afya na wateknolojia dawa kutoa elimu na kushirikiana na jamii kuhakikisha nchi inaendelea kuwa salama wakati wote.

Msasi, pia aliwataka wataalamu hao wa kada ya afya kufanya kazi kwa weledi na kutendea haki taaluma yao ili kuepuka kazi hizo kufanywa na kada nyingine ambazo hazina utaalamu wa dawa.

Alisema kuwa hivi karibuni mkoani Morogoro, alipokea taarifa ya zahanati moja inayomilikiwa na daktari iliyokuwa na stoo ya dawa, lakini haina mtaalamu wa dawa.

Alisema kuwa baada ya tatizo hilo, alitoa saa 48 zahanati hiyo itafute mtaalamu wa dawa, vinginevyo wangewapoka dawa zote.

Msasi aliwataka wateknolojia dawa hao kuwa na kauli nzuri kwa wagonjwa wanaofika kwenye madirisha ya kutolea huduma ya dawa na kuhakikisha dawa zinapatikana.

Akasema miaka kadhaa iliyopita Wafamasia walikuwa wakilaumiwa hasa pale dawa zinapokosekana na maeneo mengine kuwa na upotevu na wizi wa dawa, lakini hivi sasa wananchi wamepunguza malalamiko ya kukosa dawa badala yake wanalalamika changamoto ya bei kubwa ya dawa.

Rais wa TAPHATA, Thabiti Milandu, mbali na kuahidi kufanyia kazi maelekezo waliyopewa, alisema usugu wa dawa umekuwa unasababishwa na mambo mbalimbali, ukiwamo utumiaji holela wa dawa.

Sababu nyingine, Milandu alisema ni kutomaliza dozi ya dawa, matumizi ya dawa za binadamu kwa kutibu wanyama kama kuku na mbwa na kutupa ovyo dawa ambazo zinaingia ardhini na baadaye kunyonywa na mimea, zikiwamo mboga za majani na watu kuzila tena bila kujua.

Alisema wataalamu wa dawa wataendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa kupitia vyombo vya habari, mkutano na makongamano mbalimbali.

WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)

TPA
TANZANIA PORTS AUTHORITY

TAARIFA KWA UMMA

**MABADILIKO YA UTARATIBU WA UKUSANYAJI WA TOZO YA "WHARFAGE"**
Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inapenda kuujulisha Umma, Wateja na Wadau wa huduma za Kibandari wa ndani na nje ya Tanzania kuwa, kutokana na Mabadiliko ya Sheria, TPA itaanza tena kukusanya Malipo ya Tozo ya matumizi ya Miundombinu ya Bandari "Wharfage" kwa mizigo yote kuanzia tarehe 1 Septemba, 2024. Mabadiliko hayo yanahusisha Tozo ya "Wharfage" ambayo awali ilikuwa ikikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kutokana na mabadiliko hayo, TPA inapenda kutoa muongozo wa namna tozo hiyo ya Wharfage itakavyokuwa inakusanywa kama ifuatavyo;

**I.SHEHENA INAYOINGIA NCHINI (Import Cargo)**
Mara baada kukamilisha taratibu za kuwasilisha Kadhia ya Forodha (Customs Declaration Procedures), Mteja anapaswa kuingia kwenye akaunti yake katika Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshaji Shehena Maeneo ya Forodha "Tanzania electronic Single Window System" (TeSWS) au Mfumo wa Malipo wa TPA "TPA electronic Payment Portal" (TePP) ili kupata Ankara ya tozo ya "Wharfage" kwa ajili ya kufanya malipo. Baada ya kufanya malipo hayo, Mteja ataendelea na taratibu za kupata kibali cha kutoa mzigo (Release Order) kutoka TRA na kuweza kutoa mzigo bandarini baada ya kukamilisha malipo ya mwendeshaji bandari (Terminal Operator). Aidha ifahamike kwamba kwa Mizigo yote iendayo nje ya Nchi "Import & Transit Cargo" malipo kwa ajili ya Tozo ya Wharfage yatalipwa kwa Dola.
Ni muhimu kuzingatia kwamba, mteja hataweza kupata kibali cha kutoa mzigo (Customs Release Order) bila kukamilisha malipo ya tozo ya Wharfage.

**II.SHEHENA INAYOKWENDA NJE YA NCHI (Export Cargo)**
Baada ya kumaliza taratibu zote za kuwasilisha Kadhia za Kiforodha za upakiaji mzigo (Loading Declaration Procedures) na kabla ya kuingiza mzigo bandarini, mteja anapaswa kuingia kwenye akaunti yake katika Mfumo wa Pamoja wa Kielektroniki wa Uondoshaji Shehena Maeneo ya Forodha "Tanzania electronic Single Window System" (TeSWS) au Mfumo wa Malipo wa TPA "TPA electronic Payment Portal" (TePP) ili kupata ankara ya TPA kwa malipo ya "Wharfage". Aidha, taratibu za kiforodha za kuingiza shehena bandarini(Gate Check-in) ( zitaweza kufanyika tu pale ambapo malipo ya tozo ya "Wharfage" yatakuwa yamekamilika.

Kutokana na mabadiliko haya, TPA inatoa wito kwa Wadau na Wateja wake wote wanaohusika na uondoshaji wa Shehena bandarini kutoa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa mabadiliko haya, ili kuwezesha bandari kuendelea kutoa huduma bora kwa maslahi ya pande zote na Taifa kwa ujumla. Menejimenti ya TPA inawahakikishia Wateja, Wadau na Umma kuwa itaendelea kutimiza wajibu wake wa kutoa huduma bora wakati wote, na kushirikisha wadau wote ili kuwezesha shughuli za kibandari kufanyika kwa tija na ufanisi.

Aidha,TPA inapokea taarifa za mrejesho kuhusiana na huduma zake, kupitia njia rasmi za Mawasiliano za Mamlaka ambazo ni pamoja na Kituo cha Huduma kwa Wateja kilichopo ghorofa ya 6 katika Jengo la Makao Makuu ya TPA (One Stop Centre).

Mawasiliano pia yanapokelewa kupitia simu ya bure kwa namba 0800-110032, Barua pepe kwa anwani ya **customercare@ports.go.tz**, Tovuti **www.ports.go.tz** na kurasa rasmi za Mitandao ya kijamii za **Instagram**, **X (Twitter)** na **faceboo**k kwa jina **@tpa_tz**, kwa masaa 24.

**Imetolewa na;**
**Mkurugenzi Mkuu;**
**TPA- Makao Makuu**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge kwenye kipindi cha maswali kwake, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waliokamatwa kwa amri ya DC wafunguliwa kesi uhujumu uchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson amesema watu wanaodaiwa kukamatwa wilayani Kilombero, mkoani Morogoro kwa amri ya Mkuu wa Wilaya, wamepelekwa mahakamani na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Taarifa hiyo aliitoa jana bungeni baada ya kipindi cha 'Maswali' kutokana na maelekezo aliyotoa juzi kwa serikali kufuatilia suala hilo lililoibuliwa na Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi aliyesimama kuomba Bunge lijadili vitendo vya baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya kuwakamata wananchi na kuwaweka ndani bila sababu ya msingi na kudai kuwa hali hiyo inahatarisha haki za binadamu.

"Mfano, jambo hili limetokea jimboni kwangu Agosti 26, 2024, Mkuu wa Wilaya Kilombero akiwa kwenye ziara yake Kijiji cha Chiwachiwa, akienda kusikiliza mgogoro wa ardhi baina ya msitu wa hifadhi wa TFS (Wakala wa Misitu) na wananchi wa kijiji hicho, akiwa katika mkutano wa hadhara, diwani alitoa hoja kwa mkuu huyo kuhakiki mipaka wananchi wanaamini wapo kwenye eneo lao sahihi.

"Kauli hii ilisababisha Mkuu wa Wilaya kutoa amri ya kukamatwa kwa viongozi wa kijiji, diwani na wananchi 11 ambao hadi sasa wako ndani," alisema Kunambi.

Spika Tulia alielekeza serikali kufuatilia suala hilo, akisema kuwa Bunge litafikiria kuitazama upya sheria inayowapa mamlaka ya ukamataji wakuu wa mikoa na wilaya iwapo utekelezaji wake utabainika kutumiwa vibaya.

Katika kikao cha jana, Spika akitoa taarifa kwa wabunge kuhusu suala hilo, alisema watu hao wamefikishwa mahakamani na kufungulia kesi ya aina hiyo huku akielekeza serikali kupitia Waziri Mkuu kuendelea kulifuatilia ili kujua kesi hiyo na kosa la uhujumu uchumi limekuwapo kabla ya kukamatwa au baada ya Mbunge Kunambi kuliwasilisha na kuzungumzwa bungeni juzi.

Katika kikao hicho cha Bunge, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema serikali itaendelea kuelimisha wateule wake kutumia kwa uadilifu sheria inayowapa mamlaka ya kukamata na kuwaweka ndani watu ili kuepuka misuguano na migongano kwa jamii. Majaliwa alitoa kauli hiyo kufuatia swali la Mbunge wa Viti Maalum, Stela Fiyao, aliyedai kuwa serikali inaamini katika sheria na utawala bora ili kujenga umoja, mshikamano na upendo baina ya wananchi na serikali yao, lakini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wateuliwa wa Rais, wakiwamo wakuu wa mikoa na wilaya kutumia nguvu na mamlaka yao vibaya kukamata viongozi na wananchi na kuwaweka ndani.

Akitoa ufafanuzi wa jambo hilo, Waziri Mkuu Majaliwa alikiri suala hilo limekuwa likiibuliwa bungeni na kutolewa ufafanuzi na kwamba wataendelea kuelimisha wateule wote kwenye sheria hizo ili kuzitumia kwa weledi lakini kwa uaminifu na uadilifu kwa kufuata sheria na taratibu za nchi na kuepuka kuleta misuguano, mgongano usiokuwa muhimu.

"Jana (juzi) Kunambi (Mbunge wa Mlimba Godwin Kunambi) aliuliza suala la namna hii na Spika uliipa serikali kazi ya kufanya ya kukamilisha kutafuta majibu na naamini majibu hayo yatamjibu pia Mheshimiwa Fiyao," alisema.

Hata hivyo, alisema baadhi ya watawala kwenye maeneo yao wanazo sheria ambazo zinawaruhusu kuhakikisha hali ya utulivu na ulinzi na usalama katika maeneo yao inaimarika.



## Muheza yakabiliwa uhaba wa madawati msingi, sekondari

**Na Steven William,** MUHEZA

WILAYA ya Muheza mkoani Tanga inakabiliwa na upungufu wa madawati 7,000 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Mohamed Mfaki, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Mtoto wa Leo Samia wa Kesho uliofanyika katika Shule ya Sekondari Kwemkabara Kijiji cha Kazita, Tarafa ya Amani.

Mfaki, alisema tatizo hilo na upungufu wa vyoo ni miongoni mwa changamoto nyingi zinazokabili sekta ya elimu wilayani hapa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Zainab Abdallah, alimshukuru Rais Samia Suluhu kwa kuleta fedha nyingi za miradi ya Sekta ya elimu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Jumaa Mhina, alisema atahakikisha wanakabiliana na upungufu wa madawati ili kuwaondolea adha wanafunzi ya kukaa chini.

Awali Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Mhina, alisema wamepokea Sh. bilioni 36 kutoka serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alisema katika sekta ya elimu wametekeleza miradi 438 na kwa sasa wanafunzi wanatakiwa kuongeza ufaulu na walimu bidii katika ufundishaji.

Mkuu wa Shule hiyo, Juma Hango, alisema pamoja na mambo mengine, ufaulu katika shule yake, unaongezeka kila mwaka.

Hango, aliishukuru serikali kwa kupeleka fedha nyingi za kujenga miundombinu ya shule, ikiwamo madarasa, vyoo, maabara na ofisi ya walimu.

## Kicheba yajivunia utekelezaji miradi ya maendeleo

**Na Steven William,** MUHEZA

KATA ya Kicheba wilayani hapa Mkoa wa Tanga imetekeleza miradi ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.3 kwa kipindi cha miaka minne, imeelezwa.

Diwani wa Kicheba, Hamisi Mkodingo, aliyasema hayo wakati akisoma taarifa ya utendaji kwa kipindi hicho cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kata hiyo.

Mkodingo, alisema kiasi hicho cha Sh. 1,346,763,459.05 kimetolewa na serikali kuu, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, ofisi ya mbunge na wadau wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji Ilani ya CCM kwa kipindi hicho.

Mkodingo, alisema CCM Kicheba, inamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia kata hiyo fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kata hiyo.

Aliitaja miradi hiyo ni ya sekta ya elimu msingi, sekondari, afya, umeme, maji, barabara na ujenzi wa ofisi ya CCM.

Mwenyekiti wa CCM wa kata hiyo, Mbarouk Ayub, aliwaagiza viongozi wa chama hicho kuhakikisha kinashinda katika uchaguzi wa serikali za vijiji na vitongoji utakaofanyika nchini Novemba, mwaka huu.

# Wafugaji sasa wajikita kilimo cha mboga

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAFUGAJI jamii ya Kimasai wa eneo la Embukoi, Kata ya Donyomoruwa wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro, wameanza kujikita katika uzalishaji wa mboga za majani kwa njia ya kilimo hai ili kuepuka athari za kiafya kutokana na mazao lishe yanayozalishwa kwa kemikali.

Kundi hilo ni miongoni mwa watu 5,000 wa Kilimanjaro waliolengwa kufikiwa na Mradi wa AID-I Accelerated Innovation Delivery Initiative, unaotekelezwa na Shirika la Floresta nchini kwa kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga na Uhifadhi wa Mbegu (World Vegetable Center).

Akizungumza jana na wafugaji 116 katika shamba darasa la Embukoi, Mratibu wa Programu ya Kilimo na Mifugo wa Floresta nchini, Sinyati Ng'ida, alisema mradi huo pia, utarahisisha upatikanaji wa mbegu, uboreshaji wa lishe na mnyororo wa thamani kwa mazao ya mboga na viungo.

"Tumelenga kuwafikia watu 5,000 kwa Mkoa wa Kilimanjaro, asilimia 60 yake ni vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 29, na asilimia 45 ni wanawake," alisema Ng'ida na kuongeza kuwa:

"Mpaka sasa tumefanikiwa kutoa elimu kwa vikundi vya kuweka fedha na kukopa vijijini (VICOBA) kwa mkoa mzima wa Kilimanjaro, kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu na vikundi tofauti tofauti vya wanaotoa huduma ya kuuza chakula.

Alisema wanatarajia kuwapatia mbegu ili kuboresha lishe kuanzia ngazi ya familia mpaka shuleni.

" Pia tunatarajia kusaidia wakulima wetu waweze kuwa na mfumo mzuri wa mbegu kuanzia uzalishaji mpaka uhifadhi wa mbegu zao binafsi," alisema.

Mradi huo wa miaka miwili, unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), ulianza Januari mwaka huu na unatarajiwa kufikia ukomo Desemba mwakani.

Ofisa Kilimo wa shirika hilo, Sadock John, alisema kilimo hai kama moja ya mifumo endelevu, kina faida, pamoja na kuepusha matumizi ya kemikali, kinalinda bioanuai kwa maana ya namna viumbe wanavyoishi na wanavyotegemeana kwenye mazingira yao.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wakulima cha Kuweka na Kukopa cha Emusoi, Jackson Laizer, alisema wanaona mabadiliko makubwa katika lishe kwenye jamii yao kwa kuwa shirika hilo limewaelimisha wafugaji wa jamii hiyo kula mboga.

"Emusoi tunajishughulisha na kupanda miti, kuzalisha mboga na vitunguu, lakini jambo kubwa kwetu, hawa Floresta Tanzania, wametuelimisha Wamasai kula mboga za majani kwa sababu tulikuwa hatujui na hatutaki kula," alisema Laizer.



Ofisa Kilimo wa Shirika la Floresta Tanzania, Emanuel Ringo (kulia), akitoa elimu ya kukabiliana na magonjwa ya mboga ya mnyauko kwa wakulima wa mboga, ambao ni wafugaji wa Kimasai katika Kata ya Donyomoruwa, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu 500 wanolewa kazini

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara imewapatia mafunzo kazini, walimu wa shule za msingi ili kuwaongezea uwezo wa kufundisha wanafunzi kuanzia darasa la awali mpaka la saba.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Elimu Msingi wa halmashauri hiyo, Simon Mumbee, wakati akizungumza na Nipashe namna wanavyoboresha sekta ya elimu kuanzia darasa la awali ili kuwajengea wanafunzi umahiri wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Mumbee, alisema mpango huo unaoitwa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) ni miongoni mwa maeneo nane yanayofanyiwa kazi na Programu ya BOOST ya kuboresha elimu ya msingi.

"Tulifanya mafunzo kwa walimu wote kwa asilimia 100 Januari mwaka huu, walikuwa 551 na walimu hawa ndani yao kuna wa darasa la awali na darasa la kwanza," alisema Mumbee.

Alisema lengo kuu ni wanafunzi wa awali na darasa la kwanza wajue kusoma, kuandika na kuhesabu.

Alisema kwenye BOOST, kuna maeneo nane ya kufanyia kazi ya uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza, uboreshaji wa miundombinu na usalama wa watoto yaani shule salama, vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mengine ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), mafunzo endelevu ya walimu kazini, bajeti na utawala bora.

Mumbee, alisema halmashauri inayofanya vizuri kwenye kipengele mojawapo, inapata fedha za ziada kwa ajili ya kuboresha huduma za elimu.

Alisema kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2023 kuanzia darasa la kwanza, wanaanza kujifunza somo la Kiingereza ili kuwaongezea maarifa tangu wakiwa wadogo.

Kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), haki ya watoto wote ya kupata elimu siyo tu lengo la nne la ajenda ya mwaka 2030, bali imewekwa katika mkataba wa haki za mtoto na mikataba na matamko mengine ya kimataifa ambayo yanahitaji elimu ya msingi iwe bure na lazima kwa wote.

Mshauri wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ( PJT-MMMAM), Davis Gisuka kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), akiizungumzia BOOST, alisema inalenga zaidi elimu ya awali na kugusa moja kwa moja suala la malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Aliyataja maeneo mengine ambayo mradi unakogusa kuwa ni kusaidia kupata zana za kujifunzia kwa wanafunzi, kupunguza tatizo la ukosefu wa madarasa ya awali na kutoa mafunzo ya walimu wa awali.

Mkazi wa Babati, Daud Faustin, alisema hafahamu mradi wa BOOST ni nini ila anaona madarasa mazuri yanajengwa tofauti na zamani.





# Fuvu na koromeo vya mtoto anayedaiwa kupotea vyaokotwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

FUVU na koromeo na nguo vinavyohusishwa na mtoto wa miaka saba, Junior Maganga anayedaiwa kupotea vimekutwa katika Kitongoji cha Malenje Kijiji cha Jomu Kata ya Tinde wilayani hapa.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Diwani wa Tinde, Jafari Kanolo, alisema kuwa viungo hivyo vimeokotwa juzi baada ya mtoto huyo kupotea wiki iliyopita.

Kanolo, alisema kabla ya viungo hivyo kuokotwa juzi, siku chache zilizopita waliokota mguu wa mtoto katika Kitongoji cha Shabayanda cha kijiji hicho hicho. Alisema pembeni mwa viungo hivyo, kulikuwa na nguo za mtoto huyo ambazo inadaiwa alikuwa amevaa siku aliyopotea.

"Mtoto huyo alikuwa akisoma darasa la kwanza Tinde A (shule ya msingi), baada ya kuona viungo hivyo tulitoa taarifa polisi ambapo walifika eneo la tukio na kuondoka na viungo hivyo kwa ajili ya uchunguzi na hatua zaidi za kisheria," alisema Jafari.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga Janeth Magomi, akizungumza na Nipashe alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema wameanza kufanya uchunguzi .

"Bado tunaendelea na uchunguzi na taarifa zaidi zitatolewa kuhusiana na tukio hili," alisisitiza Kamanda Magomi.



Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Bagamoyo, Ndimbumi Joram, akitoa elimu na ufafanuzi kuhusu taarifa ya tathmini ya mazingira na jamii iliyofanywa na Kampuni ya Paulsam Geo Engineering Co Ltd katika mradi wa uchimbaji mdogo wa madini ya bauxite, ulioko Kijiji cha Magamba, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, mkoani Tanga juzi. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# DC, OCD wapinga kushtakiwa Mahakama Kuu

**Na Benny Kingson,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Tabora, Deudedith Katwale na Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) ya Tabora, Selemani Mwampamba, wamewasilisha hoja kupinga kushtakiwa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora kwa madai ya kuingilia na kuzuia amri ya Mahakama ya Baraza la Ardhi na kuomba njia mbadala itumike kumaliza.

Akizungumza nje ya mahakama hiyo, wakili wa mleta maombi dhidi ya viongozi hao kuhusu kesi hiyo, Juma Nombo, Mohamed Thabit, alithibitisha kupokea hoja hizo kutoka kwa wakili wa wajibu maombi, Samwel Muhama.

Thabiti, alidai kuwa Wakili wa Serikali, Muhama anayewatetea viongozi hao alimkabidhi hoja mbili za pingamizi juzi, lakini waliziwasilisha nje ya muda na kinyume cha sheria.

"Nimepokea hoja zao za majibu ikiwa ni pingamizi leo hii (juzi), wanadai maombi yetu hayapo sawasawa kisheria kuwashtaki DC na OCD mahakamani, tungechukua hatua nyingine kumaliza mgogoro huo, sasa sijui walitaka twende wapi? Kupata haki yetu kisheria," alidai.

Thabiti, alidai viongozi hao wamechelewa kujibu hoja zinazowakabili kisheria ikiwa ni siku 14 tangu wazipokee.

Alidai mkuu huyo wa wilaya alipokea hoja Julai 31, mwaka huu, OCD Julai 10 na wakili wao Julai 28.

Katika kesi hiyo, mkuu huyo wa wilaya anadaiwa kumwagiza OCD asitoe askari kwenda kusimamia utekelezaji wa agizo la mahakama hiyo ya ardhi kumtoa Kasawe Willa kwenye shamba lenye hekari 60 lililoko Kidatu Kata ya Mtendeni Manipsaa ya Tabora na kukabidhiwa Nombo msimamizi wa mirathi ya Asha Shaban.

"Agizo hilo linatokana na shauri la maombi madogo namba 15 la mwaka 2024 kati ya Asha Shaban dhidi ya Kasawe Willa kutoka Mahakama ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tabora na Nombo alipewa dalali Mkasiwa kutekeleza amri hiyo," alidai.

Alidai walifungua kesi hiyo dhidi ya viongozi hao namba 15946/2024 Mahakama Kuu Kanda ya Tabora chini ya Jaji Mfawidhi, Adam Mambi na kupangwa kusikilizwa juzi.

Wakili wa Serikali aliomba kupatiwa hati za ugonjwa wa mleta maombi ili kujiridhisha kwa kutohudhuria mahakamani na mwakilishi wake alete hati iliyomruhusu kusimamia kesi hiyo kisheria iliyotolewa na Msajili wa Hati Julai 24 mwaka huu.

Mwakilishi huyo, alidai Wakili wa Serikali anawapotezea muda kwa makusudi na hoja zake, na wateja wake hazina msingi, sheria ipo wazi, hivyo wanasubiri mahakama itende haki na kuwalinda.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 24, mwaka huu kutoa muda wa kuwasilishwa hati za ugonjwa wa mlalamikaji, ambaye inadaiwa yuko Dodoma kwa matibabu.

# Watoto wenye ulemavu wahakikishiwa elimu bora

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imesema itawapatia elimu bora wanafunzi wenye ulemavu ili watimize ndoto zao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Ustawi wa Halmashauri hiyo, Swaiba Chemchem, wakati akikabidhi vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi 43 wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Kahama vyenye thamani ya Sh. milioni mbili kutoka mapato ya ndani.

Chemchem, alisema wanafunzi wenye ulemavu wanahaki sawa kama wengine na ndio sababu ya halmashauri kuunda kitengo maalum kwa lengo la kuwapatia elimu stahiki kulingana na uhitaji wao.

Aliwataka wazazi na walezi kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu ndani kwa kuogopwa kuchekwa.

Mkuu wa shule hiyo, Neema Elibariki alisema vifaa hivyo vitasaidia kuondoa adha ya nyenzo za kujifunzia na kuwataka wazazi walio na watoto wenye ulemavu kuwapeleka shule.

# Mtanda ataka maboresho mkataba wa lishe

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda amewaagiza watendaji wa idara ya afya kufanya maboresho katika utekelezaji wa mkataba wa lishe ili wananchi washiriki kujenga jamii yenye afya bora.

Mtanda alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe kuanzia Julai mwaka jana hadi Juni mwaka huu baada ya kubaini watendaji katika sekta hiyo wako nyuma kwenye kutekeleza afua hiyo.

"Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na wadau tutaendelea kutekeleza afua za lishe ili kutekeleza mkataba wa lishe na kuleta tija kwa jamii ya Mwanza na taifa," alisema.

Alisema upangaji na utoaji wa fedha umeimarika kwa halmashauri kwa zaidi ya asilimia 92 na zaidi ya watoto 100,000 wamepatiwa matone ya vitamini A.

Mtanda aliionya Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuacha kutumia fedha za usimamizi wa utekelezaji wa afua za lishe katika vituo vya afya na kwa watoa huduma ngazi za jamii kwa kuwa inakwamisha mkataba wa lishe kwa mkoa.

Alizitaka halmashauri za Ukerewe na Misungwi kuongeza nguvu kwenye utoaji fedha katika shule kwa ajili ya lishe huku akiipongeza Manispaa ya Ilemela kwa kutoa zaidi ya asilimia 97 ya fedha walizojipangia.

Awali akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa afua hiyo, Mratibu wa Lishe wa mkoa huo, Sophia Lugome, alisema Mwanza ina ukondefu wa watoto kwa chini ya asilimia tano.

Alitoa wito kwa kinamama kunyonyesha watoto kwa miezi sita bila kuwapa chakula chochote na kuwapeleka hospitali wenye utapiamlo.

**Alisema upangaji na utoaji wa fedha umeimarika kwa halmashauri kwa zaidi ya asilimia 92 na zaidi ya watoto 100,000 wamepatiwa matone ya vitamini A.**



Ukurasa 12

Bilionea Afrika Kusini ampiku Dangote kuongoza utajiri Afrika



Uwekezaji pamoja na unavyotunisha mifuko kwa usalama, kuanzia mtaji Sh.10,000

Ukurasa 14


# BUFE

IJUMAA AGOSTI 30, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


### USUKANI WA UCHUMI UNAVYOSHIKWA...

# Samia anavyoendesha 'SU'; mwongozo wa Mzee Mwinyi, ubunifu na mahitaji ya leo

**Na Peter Orwa**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipozungumza na wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu wa taasisi za umma nchini (hawapo pichani), juzi jijini Arusha.. **PICHA: MAKTABA.**

KADRI muda unavyopita ndio tafsiri yake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aendako kiuchumi na mipango ya maendeleo inazidi kuwa mubashara kwa anakonuia kuufikisha uchumi wa nchi, ikiwamo eneo mahsusi mashirika ya umma.

Juzi akiwa jijini Arusha kukutana na wenyeviti wa bodi, pia watendaji wakuu wa taasisi za umma nchini, Rais Dk. Samia akafichua zaidi dhima yake kiuchumi, upande wa mashirika ya umma, maarufu 'SU'.

Hadi sasa mzizi wa anachoamua Rais, unaegemea mambo kadhaa kuanzia siasa hadi uchumi, yanayojumuishwa na mambo kama: Msukumo wa Ilani ya Uchaguzi chama chake - CCM; mipango ya taifa; kimataifa na ushauri kitaalam; mtazamo na dira yake binafsi.

Pia, kuna matukio ya kijamii kama vile maafa na magonjwa, pia mwendelezo wa mipango na yaliyoamuliwa kitaifa kihistoria, mathalani mikakati mkubwa kitaifa anayoihangaikia sasa.

Hapo umo mradi wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere, wazo lililoanza zama za serikali Awamu ya Kwanza, huku mradi wa reli ya kisasa- SGR, wazo lilianzia katika Awamu ya Nne.

Pia, katika mstari huo, majumuisho ya tafsiri ya anachoamua leo kwa mashirika ya umma, dira ya utendaji wake ina utashi na zao la nchi inakotoka kiuchumi, pia inakoelekea, ikisawazishwa na mahitaji ya sasa, chini ya usukani wa Mama.

Rais Dk. Samia akiwa muumini wa ushirikiano wa sekta binafsi na umma, maarufu PPP hoja yake ya juzi ikabeba ushuhuda wake alipochambua 'nje ndani' zilivyo, anachokihitaji kuwa mwelekeo wa taasisi hizo kitaifa sasa na kesho.

Kihistoria, msingi na mzizi wa mashirika ya umma nchini unaanzia miaka mitatu baada ya Uhuru, 1964 ulipobuniwa Mpango wa Maendeleo ya Nchi wa Miaka Mitano, ambao ni wa kwanza.

Mwaka huo 1964, pia ulianza na kuwapo mfumo hodhi kiuchumi na kisiasa, kutoka huria, hata kufungua mlango zaidi kwa 'SU' kuwa msimamizi mkuu wa biashara na uzalishaji wa kitaasisi nchini.

Ni mpango ulioitaka nchi kujitegemea na mahitaji ya msingi baada ya Uhuru, uzalishaji wake kufanywa na taasisi za nchini.

Hata wakati mpango huo ulipokuwa unakamilika mwaka 1969, tayari kulishapatikana mashirika mengi ya umma, vikiwamo viwanda vilivyoundiwa sheria na chombo cha kusimamia chini ya Ofisi ya Rais kwa jina la SCOPO.

Kwa mujibu wa Sheria ya SCOPO 1969, shirika la umma lilikuwa lenye hisa za serikali kuanzia asilimia 51 na zaidi, ingawaje katika zama hizo za uchumi hodhi, mengi yalikuwa na hisa asilimia 100.

Mageuzi ya mashirika hayo baada ya kufikia mafanikio makubwa na mapinduzi ya viwanda vya ndani, yalionekana kwa mara ya kwanza mwaka 1985, baada ya mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kisera nchini, kuelekea mfumo huria.

Ni uamuzi ambao nyuma yake ulisukuma na mageuzi ya kidunia, kwenye kusukumana dola kuu mbili; Magharibi waumini wa mfumo huria chini ya ngome yao NATO na Mashariki chini ya mfumo hodhi, wakiongozwa na iliyokuwa Jamhuri ya Muungano wa Kisovieti (USSR), wakiwa na ngome ya Warsaw Pact, wakizibeba hadi nchi za Ulaya Mashariki.

Ni bahati mbaya ngome hiyo ilianguka na dunia ikabakiwa na mbabe mmoja pekee, upande wa NATO, chini ya kiongozi wao Marekani.

Nchini katika mageuzi hayo, hatua mojawapo ilikuwa kubinafsisha 'SU', imudu kasi ya shinikizo la mageuzi kuelekea soko huria lililofunguliwa milango kitaifa.

Rais Ali Hassan Mwinyi, aliyebatizwa 'Baba wa Mageuzi' aliyajengea mazingira mageuzi, ikiwamo ya kisheria na kisera, hasa Mzee Mwinyi alipotumikia muongo wa pili wa uongozi wake, kukafanyika marekebisho mengi kisheria na kisera.

Baadhi ya mabadiliko kisheria yalitumika sana katika mageuzi hayo, mojawapo ni katika tafsiri ya shirika la umma, kubaki zinazohusika na uzalishaji au uchumi pekee.

Mageuzi hayo ya kisheria na kisera, mengi yalionekana kati ya mwaka 1991 na 1995 ikiwamo sheria nyeti za fedha, pia benki na mrithi wake, Rais Benjamin Mkapa, akayaendeleza kukamilisha mazingira yaliyoanzishwa na Mzee Mwinyi.

Rais Mkapa mwaka 1999, aliunda Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), kufaniki-

Inaendelea Uk 12

IJUMAA AGOSTI 30, 2024 BUFE 13

## UCHUMI

# Bilionea Afrika Kusini ampiku Dangote kuongoza utajiri Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

BILIONEA wa nchini Afrika Kusini, Johann Rupert, ameweka rekodi mpya ya kumpiku mfanyabiashara wa viwanda kutoka Nigeria Aliko Dangote kwa utajiri zaidi barani Afrika, kulingana na takwimu za hivi karibuni kutoka kwa taasisi ya Bloomberg Billionaires Index.

Rupert anamiliki asasi za Richemont, mojawapo ya kampuni kubwa zaidi ya bidhaa za anasa duniani, inayomiliki chapa kama vile Cartier na Montblanc.

Thamani yake sasa imepanda kwa Dola za Marekani bilioni 1.9 hadi Dola bilioni 14.3, na kumfanya kuwa katika nafasi ya 147 duniani, nafasi 12 mbele ya Dangote.

Utajiri wa bwana Dangote umepungua kwa Dola bilioni 1.7 mwaka huu na kufikia Dola 13.4, kama inavyoripotiwa na asasi ya Bloomberg.

Kushuka kwa utajiri wa Dangote kunadhihirisha ni zao la mazingira magumu ya kiuchumi ya Nigeria, kampuni zake zinakoendesha shughuli zake.

Tangu Rais Bola Tinubu ashike madaraka mwaka jana, inaelezwa ameanzisha mabadiliko kadhaa ya kiuchumi katika taifa hilo lenye watu wengi zaidi barani Afrika, ikiwa ni pamoja na kuondolewa ruzuku ya mafuta, ambayo imechangia mfumuko mkubwa wa bei, ambao kwa sasa ni zaidi ya asilimia 30.

Rais Tinubu alisema mabadiliko hayo ni muhimu, ili kupunguza matumizi ya serikali na kuchochea ukuaji wa muda mrefu.

Kuporomoka kwa kasi kwa thamani ya sarafu ya fedha Naira za Nigeria, kumemuathiri pakubwa Dangote, ambaye utajiri wake unahusishwa kwa kiasi kikubwa na mali zinazotumiwa katika sarafu ya nchi hiyo.



Aliko Dangote



Johann Rupert

Mfanyabiashara huyo mwenye umri wa miaka 66 alijipatia utajiri wake katika viwanda vya saruji na sukari na mwaka jana alifungua kiwanda cha kusafisha mafuta katika kitovu cha kiuchumi cha Nigeria, Lagos.

Himaya yake ya biashara, kundi la Dangote, pia limekabiliwa na matatizo mengi katika miezi ya hivi karibuni kutokana na kucheleweshwa kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa.

Dangote aliorodheshwa na Jarida la Forbes mwezi Januari mwaka huu, kama mtu tajiri zaidi barani Afrika kwa mwaka wa 13 mfululizo ,licha ya matatizo ya kiuchumi nchini humo.

Lakini ripoti ya hivi punde ya Bloomberg inamweka nafasi ya pili barani Afrika na ya 159 duniani.

**HANA NYUMBA UGHAIBUNI**

Dangote aliwashangaza wengi nchini Nigeria, baada ya kusema hana nyumba nje ya nchi hiyo; alikuwa na nyumba mbili - katika mji aliozaliwa Kano na Lagos.

Katika maeneo aliyoenda kwa muda, aliishi katika nyumba za kukodi, ikiwamo mji mkuu, Abuja.

Maelezo yake yaliwashangaza wengi katika nchi ambayo watu matajiri wana sifa ya maisha yao ya kifahari.

Wanigeria wengi matajiri wanamiliki nyumba katika miji kama London, Uingereza, Dubai UAE na Atlanta, Marekani.

Matamshi yake yalizua hisia nyingi kwenye mitandao ya kijamii, huku wengine wakisema ni uamuzi wa busara wa kibiashara kwani ni nafuu kulipa karo kuliko kununua nyumba.

Dangote anatoa sababu kuu ni kwamba, amekuwa akitaka Nigeria kukua kiuchumi, akifafanua: "Sababu ya kutokuwa na nyumba London au Marekani ni kwa sababu nilitaka kuangazia ukuaji wa viwanda nchini Nigeria."

Kupanda kwa thamani ya Rupert, kulichangiwa na utendaji mzuri katika sekta ya bidhaa za anasa.

Mbali na Kampuni ya Richemont yenye makao yake Uswisi, hisa zake nyingine ni pamoja na Remgro, gari la uwekezaji la Afrika Kusini lenye hisa katika makampuni zaidi ya 30, Bloomberg inaripoti.

Nicky Oppenheimer, bilionea mwingine wa Afrika Kusini, aliorodheshwa kuwa mtu wa tatu tajiri zaidi barani Afrika akiwa na utajiri wa Dola za Marekani bilioni 11.3, akifuatiwa na Nassef Sawiris, mfanyabiashara wa Misri, mwenye utajiri wa Dola za Marekani bilioni 9.48.

Mwekezaji wa Afrika Kusini Natie Kirsh alikamilisha orodha ya mabilionea watano bora wa Afrika akiwa na Dola 9.22.

Bloomberg hufuatilia mabadiliko ya kila siku katika thamani halisi ya watu matajiri zaidi duniani.

Ni kawaida, taji la mtu tajiri barani Afrika linaweza kuendelea kubadilika huku hali ya soko ikibadilika wakati biashara zikikabili changamoto tata.

Hadei, sasa Johann Rupert ni mwenyekiti wa kampuni ya bidhaa za kifahari ya Uswis Compagnie Financiere Richemont kwa mujibu wa Forbes.

Kampuni hiyo inajulikana zaidi kwa chapa za Cartier na Montblanc.

Ilianzishwa mwaka wa 1998 kupitia msururu wa mali inayomilikiwa na Rembrandt Group Limited (kwa sasa ikiitwa Remgro Limited), ambayo babake Anton aliunda katika miaka ya 1940.

Anamiliki asilimia saba ya kampuni ya uwekezaji mseto ya Remgro, akiwa ni mwenyekiti wake, pamoja na asilimia 27 ya Reinet, kampuni inayomiliki uwekezaji iliyopo Luxembourg.

Rupert amekuwa mpinzani mkubwa wa mipango ya kuruhusu fracking katika Karoo, eneo la Afrika Kusini ambako anamiliki ardhi.

- ***Kwa mujibu wa BBC.***

# SAMIA ANAVYOENDESHA 'SU'; MWONGOZO WA MZEE MWINYI, UBUNIFU NA MAHITAJI YA LEO

Inatoka Uk 11

sha majukumu makuu manne katika namna ya kuzibinafsisha 'SU'.

Kwanza, ni mashirika yaliyosuasua, hisa nyingi aliuziwa mwekezaji na sehemu chini ya asilimia 50 zikawa za serikali na wananchi waliouziwa.

Kwa mashirika yaliyofanya vibaya sana, hisa zote ziliuzwa kwa wawekezaji wayaendeleze. Aidha, kukawapo mashirika maalum kimkakati kwa uchumi wa taifa, ubinafsishaji wake ukawa wa kipindi maalum na baada ya hapo, hisa zote kurudi serikalini, nchini ilifanyika kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Aina ya nne ya mfumo huo, ni kwamba kuna baadhi ya taasisi kama vile Kiwanda cha Uchapishaji cha Taifa (KIUTA), hisa zake waliuzwa watumishi wake wanaokiendesha kiwanda, wakiwa wana mmiliki wake, maarufu kwa jina la MEBO (Management by Ownership).

Hata hivyo, mradi huo wa mageuzi kitaifa ulioratibiwa na PSRC hakufanikiwa sana, kukijumuishwa hujuma na taasisi nyingi zilizobinafsishwa, hazikutimiza malengo.

Mfano katika TRC, mwekezaji kutoka India alionyesha udhaifu ndani ya miaka michache katika mkataba wa miaka 20, hata serikali kuuvunja mkataba wake.

Ndio sura iliyotwala katika 'SU' nyingi.

Ni sababu mojwapo, eneo maarufu la viwanda Dar es Salaam wakati huo, Barabara ya Nyerere, sasa ni ya taasisi za kibiashara.

Wakati Rais Mkapa akiendesha gurudumu la mageuzi kwa mkono wa PSRC nchini, hatua hizo hazikutoa matunda makubwa kwa mageuzi yaliyotarajiwa, nyingi zilikwama, kushindwa kuhimili kasi soko la kigeni lililofunguliwa milango na baadhi zilitoweka au kubadili majukumu.

Mambo makuu kadhaa yalishuhudiwa kuwa sababu: kushindwa kuhimili nguvu ya soko la kigeni, teknolojia, mitaji, wimbi la mageuzi kidunia, uwezo mdogo wa uzalishaji kwa gharama ndogo na ubora duni wa bidhaa nchini.

**DIRA YA DK. SAMIA**

Inapoangaliwa kwa kina anachotekeleza Rais Dk. Samia leo ndani ya mageuzi ya mashirika ya umma ni matumizi ya darasa lake hasa kutoka mfumo hasa Serikali ya Awamu ya Pili na Tatu, aliyoishuhudia akiwa ameshahitimu elimu yake chuoni yenye unasaba na biashara.

Eneo mojawapo analoliweka wazi ni staili ya marehemu Rais Mwinyi wa Awamu ya Pili, kuwa na utekelezaji wa kutokukumbatia mashirika yanayosuasua, kama ilivyokuwa mwongozo wa PSRC.

Ni hoja iilyowahi kuanikizwa na Rais Mkapa alipoingia madarakani, akizama zaidi katika mitazamo iliyoasisiwa na Rais Mwinyi kuelekea mfumo huria, kwamba serikali itabaki na majukumu yake ya msingi, kuratibu biashara na uzalishaji na si kuingilia kati.

Hayo yanabeba ushuhuda wiki hii, pale Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu alipotangaza haja ya serikali kuachana na mashirika 30 hadi 40 yanayojiendesha kwa hasara, huku Rais naye juzi akatolea ufafanuzi kikaoni Arusha.

Rais akasisitiza haja ya taasisi kuwa na ubunifu katika miradi yake, akituhumu uwekezaji butu usiofanyiwa utafiti unavyoipa serikali mzigo, akitoa mifano ya majengo ya Benjamin Mkapa Tower, pia Ubungo Plaza, yote ya Dar es Salaam, kwamba ni hasara ya mtaji.

Pia akatumia nafasi ya kutetea staili ya ubunifu katika kujiendesha, akiwa na mfano wa mamlaka inayosimamia maji mkoani Tanga kufikia ubunifu wa kupanua pato kujiendesha, mwisho wake inatanua wigo wa mapato kujiendesha. Ndani ya mtazamo huo uliokuwapo katika serikali ya Awamu ya Pili, Rais Dk. Samia anahimiza mahitaji ya sasa kwa taasisi za umma, hasa watendaji wake wakuu na viongozi waandamizi, watanue wigo wa kuelewa ikiwamo kwa mafunzo, wakikaribisha ushirikiano kutoka taasisi binafsi.

Kimsingi, ni urithi unaanzia katika Serikali ya Awamu ya Nne ilipoamua rasmi kufanya kazi ya kina, aina hiyo ya uhusiano ikiwamo kibiashara, ilipopitishwa Sera na Sheria ya Ushirikiano kati ya Sekta za Umma na Binafsi (PPP).

Ndani ya mtazamo huo, Rais Dk. Samia, anazihimiza mamlaka zinazohusika serikalini, kuangalia haja ya taasisi wanazohisi tija zake ni mzigo, ama hisa kuunganishwa au kuuzwa, kurejesha uzalishaji wenye tija kimasoko.

Katika dira hiyo ikihusiana na mtaji ya umma kwa maslahi ya sasa, Rais anasisitiza kuwapo mtaji wa umma unaojitegemea, wenye tafsiri pana kwa uchumi wa sasa kitaifa na iendako, uitwao 'Sovereign Fund,' akinena ni mfumo unaotawala duniani sasa.

Hilo analioanisha na haja ya ubunifu wa kiserikali unaohitaji sasa kuvutia fedha za kigeni ndani kuingia nchini, jambo litakaloiwezesha serikali katika eneo hilo, akisisitiza mageuzi ya mashirika ya umma kuwa endelevu.

Kimsingi, wanachoelekezwa wakuu hao wa 'SU', pia utendaji wake Rais katika eneo hilo, haupo mbali na orodha ya miongozo yake kisiasa na kiutawala, kufanikisha uchumi wa nchi katika nyenzo ya taasisi hizo.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Polisi waambieni raia, ni wapi wakimbilie






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

HEBU kumbuka taarifa ya habari hii: "Mwandishi wa habari wa kituo binafsi cha runinga cha Channel Ten, Daudi Mwangosi ameuawa akiwa kwenye maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

"Mwangosi aliuawa jana katika kijiji cha Nyololo Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, kwenye maandamano ya wafuasi wa CHADEMA, huku polisi akituhumiwa kumfyatulia mlipuko."

Inapita hiyo na siku zinapita, baada ya Mwangosi kuuawa na kuzikwa kijijini kwao, watu wanalia, inatangazwa taifa limepoteza mtu muhimu, wazazi wanasaga meno na kumlalamikia Mungu wao, hatimaye inasahaulika, kifo chake kinaadhimishwa na wanahabari wenzake.

Sikiliza na hii: "Mwanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Akwilina Akwilini ameuawa baada ya kupigwa kimakosa na ofisa wa polisi aliyekuwa anatuliza maandamano ya wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

"Akwilina aliuawa jana maeneo ya Kinondoni, Dar es Salaam, akiwa ndani ya basi la abiria, maarufu daladala, ikidaiwa kuwa askari huyo alifyatua risasi kutuliza ghasia za waandamanaji, lakini ikakosea na kuelekea kwenye daladala na kumpata Akwilina."

Hisia kali zikaamka kwenye mitandao ya kijamii, wananchi wakapiga kelele, hatimaye wazazi wa Akwilina waliosema alikuwa mtoto wakimtegemea kimaisha, nao wakakata tamaa na kumwachia Mungu na kubaki na umasikini wao wa mali na mtoto. Tukatangaziwa Taifa limepoteza mtu muhimu!

Wakaiachia lawama risasi iliyofyatuliwa juu na kuingia kwenye daladala na kumpata binti wa watu, ambaye pengine leo angekuwa Ofisa Usafirishaji wa Serikali, akisaidia pia wazazi wake. Lakini waliambulia patupu masikini hao.

Wakamzika mpendwa wao na kama kawaida wakaendelea kumwomba Mungu kuwa ndiye aliyemtoa kwa hiyo hapana budi kumtwaa, wakasahau na kuangalia mambo mengine bila Akwilina kuwa karibu nao.

Baada ya kusahau tukio hilo, ikasikika taarifa ya habari nyingine: "Mlinzi wa baa, Riziki Azan ameuawa akiwa kazini. Azan aliuawa usiku wa jana akiwa kazini kwake kwenye baa hiyo iliyoko Sinza, Dar es Salaam.

"Taarifa zinasema Azan aliuawa na askari polisi aliyekuwa akisaka madada wanaojiuza na kudaiwa kuwa askari alikuwa akitaka kumkamata mmoja wa wahudumu wa baa hiyo, lakini Azan alipojitokeza kumtetea, akafyatuliwa risasi."

Wananchi waliposikia taarifa hiyo ya habari, kama kawaida wakashituka na kusikitika sana na kufuatilia, lakini wakaambiwa askari huyo alikamatwa na kufukuzwa kazi. Nadhani iliishia hapo huku Azan akizikwa na ndugu zake na mambo kubaki kumwomba Mungu tu kwa kumpenda zaidi.

Tukaambiwa Taifa limepoteza mchapakazi.

Taarifa za habari zipo kila siku, mara tukasikia na hii: "Kijana mhitimu wa kidato cha sita, Meshack Daudi ameuawa Lamadi, mkoani Simiyu baada ya askari polisi kuwafyatulia risasi waandamanaji waliokuwa wakipinga matukio ya watoto kutekwa."

Wazazi wa Meshack wakashituka kusikia kuwa mtoto wao aliyekuwa amefaulu mitihani ya kidato cha sita na kupata Daraja 1, akitarajia kujiunga na chuo kikuu, tayari hayupo duniani anajiunga na wenzake ahera!

Serikali ikatangaza kuwa itagharimia mazishi na maziko ya kijana huyo pamoja na matibabu ya wengine waliojeruhiwa kwenye kashkashi hilo. Sidhani kama gharama hiyo itawaweka sawa wazazi wa mkombozi mtarajiwa huyo wa familia!

Baada ya taarifa hizo, kikawa kinafuata kipindi cha Usalama wa Raia redioni. Wananchi wakifundishwa umuhimu wa kuwa na Jeshi la Polisi lenye dhima ya kulinda usalama wa raia na mali zake kwa weledi na uadilifu mkubwa.

Wakieleweshwa jinsi Polisi inavyokuwa kimbilio lao wapatapo matatizo, wakiambiwa kuwa askari hapaswi kutumia nguvu za ziada akamatapo au atulizapo ghasia, bali kauli na elimu viwe kipaumbele.

Kwamba risasi itatumika pale tu kunapotokea mtafaruku unaohatarisha maisha ya askari mhusika na lakini pia ifyatuliwe angani na si kulenga mtu moja kwa moja, isipokuwa tu anapokuwa na silaha akimlenga askari.

Lakini hakuna mahali ambako kunasema risasi hizo kuna nyakati zikilengwa juu hukaidi na kugeuza njia na kwenda mshazari na kumpata yeyote awapo mbele yake. Kwamba haziwezi kutii sheria bila shuruti.

Jeshi la Polisi hivi sasa linalalamikiwa sana nchini, kutokana na kuhusishwa na masuala mengi kama haya... Hivi kweli jamani? Ni lipi kimbilio la raia sasa?

FEDHA

# Uwekezaji pamoja unavyotunisha mifuko kwa usalama, kuanzia mtaji wa Sh.10,000

**Na Beatrice Moses**

FURSA ya uwekezaji wa kuanzia Sh 10,000 inayopatikana kwenye mifuko kadhaa ya uwekezaji wa pamoja ikiwamo Faida Fund, inaendelea sasa kuwavutia wananchi kwa kuaminika, ikihusisha taasisi zinazotambulika na kuaminika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investments (WHI) Dk. Fred Msemwa, waendeshaji wa Mfuko wa Faida, anasema Watanzania 900,000 ndiyo wanaowekeza kwenye maeneo tofauti, ikiwamo mfuko wao uwekezaji pamoja kipato cha ziada, kwa kipindi kifupi au kirefu kwa faida ya ukwasi madhubuti.

Dk. Msemwa anatumia nafasi hiyo, akieleza mfuko wao wa uwekezaji unatoa fursa kwa taasisi na watu binafsi kuwekeza kipato chao cha ziada kwa kipindi kifupi, cha kati au muda mrefu kwa faida ya ukwasi madhubuti.

Ulianzishwa Novemba 2022, kwa mauzo ya vipande yalianza rasmi Januari mosi,2023. Mahitaji ya awali ya uwekezaji ni Sh 10,000.



Wanajamii katika vikao vya vikundi vya kukopeshana. **PICHA: MTANDAO**

Katika mfuko huo, mwekezaji anaruhusiwa kuchukua fedha yake wakati wowote baada ya kukamilika kwa siku 90 tangu alipowekeza mara ya kwanza, malipo hufanyika ndani ya siku tatu bila ya kutozwa gharama ya kutoa.

Anasema wakati akitoa taarifa ya mwaka ya Mfuko wa Faida Fund kwa mwaka wa fedha unaoishia 23 Juni 2023 iliyotolewa kwenye Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wawekezaji wa Mfuko huo, uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Katika mkutano huo, ikaazimiwa kuongeza wigo wa uwekezaji kwa kutoa elimu ya hamasa katika maeneo tofauti nchini ikiwamo vyuoni na vijijini kwa wakulima, kwa kuwa uwekezaji katika mfuko huo ni rahisi unatumia simu ya mkononi, pia umeunganishwa na mfumo wa malipo ya serikali.

"Faida ya kuwekeza kwenye mfuko huu ni kubwa kwa kipindi cha miezi 8 ya mwanzo kilichoishia 20 Juni mwaka 2023 ilikuwa asilimia 10 imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 12 ya mwaka ulioishia 30 Juni 2024.

"Hivyo faida iliyopatikana ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 9.7 dhamana ya serikali ya miaka mitano," anasema Dk. Msemwa.

Thamani ya mfuko huo imekuwa na kufiia Sh. bilioni 25.96 kutoka Sh. bilioni 15.35sawa na ongezeko la asilimia 41. Wakati thamani ya kipande imeongezeka na kufikia Sh, 115.8120 kwa kipande Juni 30, 2024 kutoka Sh, 104.9707kwa kipande kwa taarifaya Juni 30, mwaka 2023.

Ongezeko la ukuaji wa mfuko huo inaelezwa kuwa linatokana na ongezeko la idadi ya wawekezaji kwa kipindi kinachoishia 31 Juni 2023 ilifikia 2,041 hadi kufikia Juni 2024 imefikiwa wawekezaji 4,806 sawa na ongezeko la asilimia 58 ya waliopo.

Anasema uwekezaji kwenye mfuko huo unaanzia Sh. 10,000 hivyo mtu yeyote mwenye kipato kuanzia kidogo, cha kati na juu anaweza kuwekeza na kuvuna faida inayopatikana inayotokana na thamani ya vipande iliyopo kwenye soko kwa wakati huo.

**WAWEKEZAJI**

Mmoja wa wawekezaji katika mfuko huo Elizabeth Michael, anayejitambulisha mtumishi wa serikali mkoani Tanga, amewekeza kwenye mfuko huo akijiandalia maisha ya kueleweka wakati atakapostaafu, anahamasika kwa faida ya gawio anayoiona tangu alipoanza kuwekeza mwaka jana.

Mwekezaji mwingine Meshack, Mafyeko, ambaye ni Mkurugenzi wa Voice of Eagle Tanzania, anasema wamejikabidhi jukumu la kuhamasisha wasichana waliopo kwenye mradi wa Binti Mwenye Ndoto na uwekezaji kuwekeza kwenye mfuko huo kwa kuwa wanauamini.

> **"Faida ya kuwekeza kwenye mfuko huu ni kubwa kwa kipindi cha miezi 8 ya mwanzo kilichoishia 20 Juni mwaka 2023 ilikuwa asilimia 10 imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 12 ya mwaka ulioishia 30 Juni 2024.**

Anasema, kuna mabinti kadhaa katika mradi huo ambao hujifunza ushonaji kisha hufanyiwa utaratibu wa kupewa cherehani ili kumudu kuanza kujitegemea, lengo ni kuwawezesha kukuza kipato chao, hivyo njia nyingine ambayo wameibaini inaweza kuwasaidia wasichana hao ni kuwekeza.

"Shida inayowakabili watu wengi ni kukosa elimu ya fedhanauwekezaji, mfumo wa mitala yetu ya elimu haisaidii mwanafunzi kujifunza hayo kwa wakati, sisi tumeamua kutoa elimu hiyo kwa wale tunaowafikia ili waweze kupiga hatua katika maendeleo ya kipato chao," anasema.

Anasema kuwa mwekezaji siyo lazima kuwa na mamilioni ya fedha unaanza kuwekeza kidogo kwa malengo, kama Mfuko wa Faida unatoa fursa ya kuwekeza kuanzia Sh elfu 10.

Mwalimu wa masuala ya Fedha, Amina Ramadhani, anasema kuna haja kuwahamasisha vijana kuwekeza kwenye matumizi mazuri ya fedha, ikiwamo kuwekeza kwenye taasisi zinazotambulika kama kumiliki vipande vya mifuko ya aina Faida Fund.

Anahmaiasha vijana ya kutumia fedha zao kwenye mambo yasiyowaletea maendeleo ya kiuchumi, ni vyema wakajikita katika miradi inayoangukia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji ya Dhamana(CMSA).

"Uwekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja ni njia mbadala ya kuwekeza kwenye masoko ya mitaji, mifuko hii huwezesha mwekezaji kutawanya uwekezaji wake sehemu mbalimbali kulingana na sera ya mfuko," inaelezwa kwenye mwongozo huo.

Mifuko hiyo, pia husimamiwa na wataalamu wenye uzoefu wa uwekezaji, hivyo kusaidia kupunguza uwezekano wa kupata hasara katika uwekezaji.

"Mifuko ya uwekezaji wa pamoja pia ina faida ya kuwezesha wawekezaji wenye akiba kidogo kuwekeza kwani bei ya vipande ni ndogo inayoweza kulipiwa na wenye vipato vya chini na wasioweza kushiriki kwenye masoko ya mitaji moja kwa moja," inaelezwa.

Faida nyingine anaitaja ni kwamba, mapato yatokanayo na uwekezaji kwenye mfuko hayatozwi kodi ya zuio wakati viwango vya riba za mabenki ni kaba ya kutoa kodi ya zuio.

Dk. Msemwa anabainisha kuwa kwenye mfuko wa Faida, unaruhusu wawekezaji kuuza vipande vyao wakati wowote baada ya kumaliza siku 90 tangu mwekezaji alipowekeza hivyo anaweza kupata fedha zake kama anazihitaji baada ya ipindi hicho.

"Hakuna gharama za kuingia(kuwekeza) au kutoka(kuuza vipande) katika mfuko uwekezaji Faida Fund hauna muda maalum wala ukomo, mwekezaji anaweza kutumia vipande alivyowekeza kama dhamana ya kupata mkopo benki,"anasema.

Pia Faida Fund inatoa suluhisho la uwekezaji kwa makundi maalum ikiwamo wastaafu, watoto, wawekezaji wa pamoja,hivyo kwa ujumla kuna faida zaidi ya kuwa na amana kwa sababu inamuongezea mhusika kipato kikubwa kutokana na viwango bora vya faida na fursa nyinginezo.

Mgawanyo wa uwekezaji kwenye mfuko huo umewekeza zaidi kwenye dhamana ya muda mrefu kwa kiasi cha asilimia 91, asilimia tau ni kwa amana za benki za muda malum na asilimia sita imewekezwa kwenye amana za benki za mda mfupi.



## Viongozi, wadau waombwa kushirikiana

**Na Peter Mkwavila,**
CHAMWINO

MKURUGENZI wa Shirika lisilo la Kiserikali la Foundation for Disabilities Hope (FDH), Maiko Salali, amewaomba viongozi wa serikali na dini wa kata, vijiji na vitongoji kushirikiana na wadau wa elimu ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa wanawake na watoto wenye ulemavu nchini.

Salali alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na viongozi wa serikali na dini wa Kata ya Buigiri wilayani Chamwino Mkoa wa Dodoma kwenye uzinduzi wa mradi wa kupinga ukatili kwa wanawake na watoto wenye ulemavu unaofadhiliwa na Shirika Women Fund Tanzania Trust.

Aliwaomba viongozi hao kushirikiana na wadau ambao wamekuwa wakifadhili miradi kwa malengo ya mapambano dhidi ya vitendo vya kikatili wanavyofanyiwa watoto na wanawake wenye ulemavu.

Alisema mradi huo umejikita kutoa elimu ya mapambano dhidi ya vitendo hivyo viongozi wa serikali washirikiane na wadau hao ili walemavu waweze kupata haki zao za msingi.

Mkurugenzi huyo, alisema shirika hilo limekuwa likisaidia watu wenye ulemavu kuwafanya kuwa na uwezo wa kuvunja vikwanzo vinavyosababisha kushindwa kupata haki zao ikiwamo watoto kutopata elimu inayostahili.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Chamwino, Zaina Msangi, alisema serikali kupitia viongozi wake wataendelea kushirikiana na wadau kukomesha vitendo hivyo wanavyofanyiwa wanawake na watoto wenye ulemavu.

Alisema halmashauri hiyo itahakikisha ufadhili huo waliopata viongozi wanashirikiana na wadau ili malengo yaweze kufikiwa.

Diwani wa Viti Maalum Kata ya Buigiri, Saada Omar, aliwataka wadau wanaofadhili miradi kwa ajili ya makundi mbalimbali kutimiza malengo yao kwa kuwafikia wenye mahitaji.

Alisema mahitaji bado ni mengi kwa watu wenye ulemavu, hivyo kupitia mashirika na taasisi ambazo zimekuwa zikifadhili mchango wao unahitajika ili kuwakomboa wenye changamoto.

# Madiwani Mkalama wachachamaa mabomba kutoa maji machafu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida wamekuja juu na kumwagiza Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA) kuomba msaada Wizara ya Maji wa kulipatia ufumbuzi wa tatizo la maji machafu kutoka kwenye bomba ili kunusuru afya za wananchi.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, James Mkwega, wakati wa kikao cha baraza la madiwani cha robo ya nne.

Ni baada ya madiwani kuhoji sababu tatizo la maji katika mradi wa maji Ibada kutopatiwa ufumbuzi kwa muda mrefu na wananchi kuendelea kupata maji machafu, hivyo kuhatarisha maisha yao.

"Meneje RUWASA kama ngoma hii imewashinda si muombe msaada Wizara ya Maji, haiwezekani kila kikao cha baraza tunachokutana suala la maji mabomba kutoa machafu kata ya Ibaga linaibuka," alisema.

Diwani wa Ibaga, Salum Lindi, alisema tatizo la mradi wa kisima cha maji Ibaga kutoa maji machafu ambayo ni hatari kiafya limekuwa la muda mrefu na halipatiwi ufumbuzi.

"Tatizo la maji kutoka machafu ameshafika Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Singida, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mkalama, lakini wataalamu wanasema tatizo limeshughulikiwa wakati maji bado yanaendelea kutoka machafu," alisema.

Huku akionyesha sampuli ya maji hayo ambayo aliingia nayo kwenye kikao hicho na kukabidhi kwa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo.

Lindi, alisema majibu kwamba mabomba ya maji ya mradi huo yatakuwa yamechafuka ndio maana yanatoa maji machafu sio kweli.

Alisema mradi huo una miaka mitatu tangu ujengwe wakati ipo miradi yenye zaidi ya miaka 15 maji yanatoka masafi na sio machafu kama hayo.

Diwani wa Mpambala, Boaz Ndanduto, alisema majibu ya wataalamu kuhusu tatizo hilo ni ya kubahatisha kwani hayana uhakika na ndio maana tatizo hilo limedumu kwa miaka mitatu.

"Wataalamu wanasema inawezekana labda hivi, kwanini wasitoe jibu ambalo tunaweza tukawapelekea wananchi kule wakatuelewa, " alisema.

Diwani wa Kinampundu, Habiba Hamis, alisema tatizo la maji kutoka machafu katika kata hiyo ni la muda mrefu, lakini wataalamu hawatoi majibu ya uhakika na kushinikiza jana wapewe majibu yanayojitosheleza.

"Leo (jana) tunataka tupate majibu ya kujitosheleza maana maji ni uhai haiwezekani watu wakawa wanatumia maji kama haya ambayo utafikiri ni petroli, mafuta ya kula, hatuwatendei haki wananchi wa Ibaga," alisema.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mkalama, Lameck Itungi, aliwataka wataalamu watumie mbinu kutatua tatizo hilo ili kuhakikisha linapatiwa ufumbuzi kwani chama hicho kinataka kuona wananchi wanapata maji safi na salama.

Meneja wa RUWASA wa Wilaya hiyo, Omary Matembo, akijibu malalamiko hayo alisema baada ya kupata ripoti ya kuwapo kwa maji machafu Mei mwaka huu, timu ya wataalamu wa RUWASA kutoka mkoani na wilayani walifika Ibaga kufanya uchunguzi.

Matembo, alisema baada ya kufuatilia, walibaini maji yaliyokuwa yanatoka kwenye tangi la kuhifadhia maji yalikuwa masafi, lakini kwenye mabomba kwa baadhi ya wateja yalikuwa yanatoka machafu.

Alisema uchunguzi zaidi ulibaini kuwa, njia za mabomba zilikuwa zimejaa uchafu na kufanyiwa usafi kwa muda wa wiki mbili na baadaye maji yakaanza kutoka masafi.

Aliwaomba madiwani wapewe muda wafuatilie zaidi ili kubaini changamoto gani imejitokeza.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Chang'ombe, jijini Dodoma, Bashiri Kitakata, akizungumza wakati wa mkutano wa hadhara katika viwanja vya Kanisa la Pentecost Christian International, Mtaa wa Mji Mwema jana wa kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuhakiki majina yao kwenye daftari la mpigakura, ili waweze kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, pamoja na kuuombea ili ufanyike kwa amani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wananchi watahadharishwa homa ya nyani

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WANANCHI wametakiwa kuchukua tahadhari kwa kuepuka misongamano, kugusana na ngono zembe ili kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa homa ya nyani maarufu kama monkey pox.

Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Dharura wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Dharula, George Dilunga, alitoa wito huo jana wakati akitoa tahadhari juu ya ugonjwa huo.

Dk. Dilunga, alisema wananchi wanatakiwa kuepuka kusalimiana kwa kugusana ili kuweka tahadhari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

"Tunawe mikono yetu kwa maji tiririka kila mara ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huu," alisema.

Alisema Idara ya Magonjwa ya Dharura ya BMH imejipanga endapo watapokea kesi ya ugonjwa huo ambao hadi sasa hauna tiba."Mfano mgonjwa ana homa, basi tunatibia ile homa. Mgonjwa pia anakuwa na shida ya ngozi hasa kuwa na vipele vinavyotoa majimaji kama tete kuwanga," alisema Dk. Dilunga.

Alisema ugonjwa huo umeanzia Afrika ya Kati na kuwa mpaka sasa Tanzania haina rekodi ya kupata mgonjwa yeyote mwenye maambukizi ya ugonjwa huu.

Alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni homa, kusikia baridi, maumivu ya mgongo, misuli, kichwa, kuvimba koo, kupata vidonda kooni na kikohozi.

Dilunga alifafanua kuwa ugonjwa huo unaambukiza kupitia virusi na kuathiri viungo kwa kudumu kama hautatibiwa mapema.



# Wafanyakazi, wazabuni waidai halmashauri Chunya bilioni 2.1/-

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya inadaiwa zaidi ya Sh. Bilioni 2.1 kwa kulimbikiza malipo ya mishahara ya watumishi, wazabuni, watoa huduma, stahiki za watumishi ikiwemo matibabu na likizo.

Mweka Hazina wa Halmashauri hiyo, Rajabu Lingoni aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha kufunga mwaka wa fedha uliopita wa 2023/2024.

Lingoni, alisema baadhi ya madeni hayo yanapaswa kulipwa na serikali kuu na mengine fedha za mapato ya ndani.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 260 ni malimbikizo ya mishahara ya watumishi, Sh. milioni 145 madeni ya wazabuni na watoa huduma, Sh. milioni 716 stahiki za watumishi ikiwemo matibabu, likizo, uhamisho na gharama za mafunzo na Sh. milioni 630 ukopeshaji kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema halmashauri hiyo, ilishindwa kulipa baadhi ya madeni hayo kutokana na kukosekana kwa vifungu na wanakusudia kulipa mwaka huu wa fedha wa 2024/2025.

"Baadhi ya madeni haya tunakusudia kuyalipa kwa kutumia fedha za bakaa, mpaka tunafunga mwaka halmashauri yetu imebakiwa na bakaa ya Sh. Bilioni 1.7 kwa hiyo baadhi ya madeni ambayo tulishindwa kuyalipa kwa sababu ya kukosekana vifungu tutalipa," alisema Lingoni.

Alisema halmashauri hiyo imevuka mwaka ikiwa inawadai baadhi ya watu zaidi ya Sh. milioni 300.

Mkuu wa wilaya hiyo, Mbarak Batenga, aliiagiza halmashauri hiyo kuanza kulipa madeni hayo hasa kuhusu stahili za watumishi.

Batenga, alisema kitendo cha kuchelewa kuwalipa stahiki hizo kinaweza kikawa chanzo cha kushuka kwa morali ya utendaji kazi.

Alisema pamoja na kukosekana kwa vifungu vya kulipia madeni hayo, halmashauri ilikuwa na uwezo wa kubadili matumizi ya baadhi ya vifungu kwa kuvielekeza kwenye ulipaji wa madeni ili kuepuka madoa ya madeni.

Alisema kitendo cha kuvuka na deni la zaidi ya Sh. Bilioni 2.1 kinaweza kukaisababishia halmashauri hiyo matatizo.

Aliwataka watendaji kusimamia vizuri vifungu ili ukusanyaji wa mapato uendane na ulipaji wa madeni.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka aliwashauri watendaji wa halmashauri hiyo kuwa makini wakati wa kuandaa vifungu vya matumizi ili kuepuka visiishe kabla ya wakati na kusababisha kushindwa kulipa madeni.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Bosco Mwanginde, aliwataka watendaji wa halmashauri kuendelea kushirikiana na madiwani ili kuhakikisha malengo yanayowekwa yanafikiwa.

Aliagiza vifaa vyote vya halmashauri hiyo yakiwemo magari mabovu kupigwa mnada kwa mujibu wa sheria ili kuepuka hoja kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG)..



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Mbarak Batenga, akisisitiza jambo alipokuwa anatoa salamu za serikali katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya wilaya hiyo cha kufunga mwaka wa fedha 2023/2024, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Afa kilabuni akinywa pombe na wenzake

**Na Gideon Mwakanosya,**
RUVUMA

MKAZI wa Ruhuwiko Manispaa ya Songea mkoani hapa, Joseph Ndomba (52) maarufu kwa jina la Manyota, amefariki dunia katika kilabu cha pombe za kienyeji.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Alfred Husseini alisema kuwa tukio hilo lilitokea juzi asubuhi katika Mtaa wa Ruhuwiko Shuleni kwenye kilabu hicho kinachomilikiwa na Osana Mbele wakati yeye na wenzake wakinywa mbege na komoni.

Husseini, alisema mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi na sampuli ya pombe imechukuliwa na kupelekwa kwa mkemia mkuu wa serikali kwa uchunguzi zaidi.

Alisema polisi wanamshikilii muuzaji wa pombe ambayo marehemu na wenzake walikuwa wanakunywa kwa mahojiano zaidi ili kubaini chanzo cha kifo hicho.

Ametoa wito kwa wananchi hasa wale wanaotumia vileo kuepuka kunywa pombe zilizotengenezwa kienyeji kwa kuwa hazijathibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kuepuka madhara yanayo weza kujitokeza.

**Husseini, alisema mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi na sampuli ya pombe imechukuliwa na kupelekwa kwa mkemia mkuu wa serikali kwa uchunguzi zaidi.**

# TANROAD, TARURA waagizwa kujenga barabara maeneo ya uwekezaji Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amewaagiza Wakala wa Barabara (TANROAD) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani hapa kupeleka barabara katika maeneo yenye uwekezaji mkubwa.

Mtaka alitoa agizo hilo juzi kwenye kikao cha bodi ya barabara kilichohusisha taasisi zote za umma kilichofanyika mjini hapa.

Mtaka alisema ili kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani katika halmashauri ni lazima serikali iboreshe miundombinu ya barabara, madaraja, umeme na maji katika maeneo yanayozalisha mazao ya misitu, chai na parachichi.

"Lazima tuweze kujua tuna maeneo yanayozalisha ili taasisi zetu ziweze kufanya kazi kwa sababu ndiko hela zinakotoka, kwa hiyo unapoandaa miradi kwa mkoa kama Njombe tunatamani umeme uende asilimia 100 kwenye vijiji na mashamba yao," alisema.

Alisema taasisi hizo zinapaswa kutoka katika kufikiri kwamba miundombinu inahusu binadamu pekee badala yake huduma hizo ziende katika maeneo ambayo kuna uzalishaji.

"Watu leo wangetamani wafungue mashamba ya parachichi wafunge mifumo ya umwagiliaji lakini maji hakuna," alisema.

Meneja wa TANROAD Mkoa wa Njombe, Ruth Shalua, alisema kupitia mpango kazi wa mwaka 2024/25, mkoa umepangiwa Sh. Bilioni 15.8.

"Katika vyanzo vyetu vya mapato kuna fedha tutazipata mfuko wa barabara jumla ya bilioni 11.5 na mfuko wa maendeleo bilioni 4.27 na mpaka sasa tunazo fedha, " alisema.

Alisema wana mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kibena-Lupembe hadi Madeke kilomita 126 na sehemu ya Kibena-Kidegembye kilomita 42.

Meneja wa TARURA wa mkoa huo, Gerald Matindi, alisema wamejipanga kuingiza fedha kwa ajili ya kufungua barabara katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wa Mkoa huo, Wilson Novath, alisema kwa mwaka wa fedha, wametengewa bajeti ya shilingi Bilioni 7.6.

"Tuna programu maalumu ya uchimbaji visima kwa Mkoa wa Njombe tuna visima 25, fedha tunazo tutaanza mwezi huu wa Septemba," alisema Novath.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Agnetha Mpangile, aliwaomba TARURA kutengeneza barabara ya Utalingolo, Ihalula na Nole kwa kuwa kuna maeneo yanayozalisha kwa kiwango kikubwa mazao ya misitu.



# Bilioni 11.7/- kukarabati majengo ya shule

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHILINGI bilioni 11.7 zinatarajiwa kutumika kwa ukarabati wa majengo ya shule 22 za visiwani hapa.

Hayo yalibainika jana wakati Mkuu Kikosi cha Kupambana na Kuzuia Magendo (KMKM), Komodo Azani Hassan Msingiri akikagua ukarabati wa majengo ya Shule ya Mwera Regeza Mwendo.

Msingiri, uamuzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwapa kazi ya kukarabati majengo ya shule hizo ni moja ya mafanikio na kazi nzuri inayofanywa na kikosi hicho.

Alisema fedha hizo zitatumika ili kuwa na majengo yenye viwango kwa vile kikosi hicho kina mafundi wabobezi wa kazi hiyo.

Alisema serikali ina lengo la kuwekeza katika elimu na elimu bora haipatikani ikiwa hakutakuwa na majengo yenye viwango vya ubora.

Msingiri, alisema kikosi hicho kinashinda zabuni za ujenzi kwa kuwa kinafanya kazi kwa weledi na kuendelea kujenga imani kwa serikali na wananchi.

Msimamizi wa ukarabati wa majengo hayo, Saleh Ali Saleh, alisema wanatarajia kukamilisha kazi hiyo Oktoba mwaka huu ili wanafunzi wa shule hiyo waendelee na masomo.

Salehe, alisema ukarabati wa unahusisha madarasa 19 na ofisi za walimu na kuwataka wananchi kuwa walinzi na kuitunza miundombinu ya elimu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Khamis Salum Khamis, alisema ukarabati huo ni muhimu kwa kuwa majengo yalikuwa chakavu na kuhatarisha maisha ya wanafunzi na walimu.

**Msingiri, uamuzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwapa kazi ya kukarabati majengo ya shule hizo ni moja ya mafanikio na kazi nzuri inayofanywa na kikosi hicho.**

# Serikali kuongeza wigo uwekezaji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali inatarajia kuongeza wigo wa uwekezaji kwa sekta nyingine ikiwamo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutokana na Zanzibar kupata mwamko mkubwa wa kupata maendeleo. Soraga alitangaza mpango huo

visiwani hapa jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa mwanzo wa jukwaa la jopo la Watendaji Wakuu wa taasisi binafsi katika uwekezaji kwenye sekta ya utalii.

Alisema jukwaa hilo ni nzuri maana hata wawekezaji wanapotaka kuja kuwekeza nchini jambo la mwanzo kuuliza kama kuna jukwaa lolote la makampuni ili kupata uzoefu.

Alisema uwapo wa jukwaa hilo itazidi kuipa heshima Zanzibar kuwa ni sehemu sahihi na salama kwa ajili ya uwekezaji kwa kuwa kuna mjumuiko wa wakuu wa taasisi na jukwaa lao.

Alisema serikali inaunga mkono na kulipokea jukwaa hilo na kutoa wito kwa wakuu hao kuwa lisiishie tu katika vikao badala yake kwenda serikalini kuonesha njia bora za kutumia kuvutia kwa wawekezaji, kuboresha uwekezaji na biashara.

"Pia, kuangalia masuala ya viwanda vidogo vya kuongeza samani, mawasiliano, biashara za usafiri na uchukuzi hayo ni maeneo ambayo bado kwa upande wa kisiwa hatufanyi vizuri," alisema Soraga.

Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi wa sekta binafsi wa Zanzibar, Dk. Jocephine Rogate Kimaro, alisema jukwaa hilo linawakutanisha maofisa watendaji wakuu kutoka sekta binafsi kujifunza na kuhakikisha wanapeana ushirikiano kukuza biashara zao.

"Kama mnavyofahamu katika utendaji kuna changamoto mbalimbali na si rahisi kuzizungumza katika taasisi husika, lakini wakikutana kupitia mikutanoni watapeana ushauri katika changamoto zinazowakabili," alisema Dk. Kimaro.

Alisema jukwaa hilo ni muhimu kutatua changamoto wakati huu uchumi wa Zanzibar unakua na kuleta matokeo chanya.

Alisema moja ya mambo ambayo jukwaa hilo linaweza kujadiliana ni jinsi ya kukuza brandi zao, mitaji yao na kutatua masuala yanayohusiana na ajira, sheria na taratibu mbalimbali katika fursa za uwekezaji.

Alisema inahitajika kufanya tafiti wa wakuu wa taasisi binafsi wanawake ili kuwasaidia kufanya mamauzi sahihi wakati wa kukuza biashara zao na kuongeza idadi yao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Ajira na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif, alisema kuanzishwa kwa jukwaa hilo ni jambo muhimu kwa uchumi wa nchi na nia ya serikali ni kuhakikisha sekta binafsi inakua kwa kuwa na makampuni makubwa.



Meneja Uhusiano Mwandamizi Sekta ya Umma na Taasisi wa Benki ya NBC, Gasto Ndanu (wa pili kulia) na Meneja Uhusiano Huduma Binafsi wa benki hiyo, Khafsa Mohammed (kulia), wakijadiliana jambo na baadhi ya wadau wa sekta ya biashara, wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Kimataifa la Wakuu wa Mashirika na Kampuni Zanzibar, uliodhaminiwa na benki hiyo, juzi jioni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sita kortini kwa kusafirisha karafuu kwa magendo

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumi Uchumi Zanzibar (ZAECA) Mkoa wa Kaskazini Pemba imewafikisha mahakamani watu sita kujibu mashtaka ya kusafirisha karafuu kwa njia ya magendo.

Washtakiwa hao, Yusuf Mohamed Juma (26), Omar Haji Nassor (32), Kombo Juma Haji (28), Hamad Rajab Juma (30), Haji Issa Haji (48) na Abeid Suleiman Ali (48), wakazi wa Wambaa walifikishwa jana katika Mahakama Kuu ya Zanzibar iliyopo Chake Chake Pemba.

Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Juma Ali Juma mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Salum Hassan Bakar alidai kuwa, washtakiwa hao walitenda kosa hilo Novemba 13 mwaka jana saa 10:00 alfajiri katika Kisiwa cha Yambo na Sahare Tanga.

Juma, alidai washtakiwa hao walikamatwa na kilo 1,534.5 za karafuu kavu zenye thamani ya Shilingi milioni 20,047,750 baharini wakati wakisafirisha kinyume cha sheria.

Washtakiwa hao walikana mashtaka hayo na kuachiwa baada ya kutimiza masharti ya dhamana kwa kila mmoja kwa Sh. milioni nne na wadhamini wawili wenye kiasi kama hicho na vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi.

Jaji Bakar aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 19, mwaka huu, itakapotajwa tena.



Diwani wa Kata ya Mtekente, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, Noel Shole, akinywa maji ya kisima kilichochimbwa na kampuni ya kiwanda cha pamba cha BiosustainTanzania Ltd katika Shule ya Sekondari Mtekente, wilayani humo juzi. Kampuni hiyo, pia imetoa msaada wa vitanda na magodoro na kujenga bweni na jiko shuleni hapo, kwa gharama ya Sh. milioni 180. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wanafunzi wakombolewa mwendo kilomita 20 kwa kujengewa bweni

**Na Thobias Mwanakatwe, IRAMBA**

WANAFUNZI wa kike wa Shule ya Sekondari Mtekente wilayani Iramba mkoani Singida, wameondokana na adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 20 kwa siku baada ya kujengewa bweni.

Meneja Miradi wa Biosustain Tanzania Limited, Tawanda Mutonhori, akikabidhi bweni hilo kwa viongozi wa kata hiyo, alisema kampuni hiyo kwa kushirikiana na Cotton Made in Africa (CmiA) ya nchini Ujerumani wamefanya hivyo ili kuunga juhudi za serikali za kumwinua mtoto wa kike.

Mutonhori, alisema wamejenga bweni hilo kutokana na changamoto wanazopitia wanafunzi wa kike kwa kutembea umbali huo mrefu kutoka nyumbani kwao kwenda shule na kurudi huku wengine wakipanga mitaani hali iliyokuwa ikisababisha utoro na wengine kuacha shule.

"Kampuni imeweza kujenga bweni lenye uwezo wa kubeba wasichana 80, vitanda 40 na magodoro. Pia, imejenga jiko kwa ajili ya kupikia chakula, mabafu ya kisasa 10 yenye sehemu ya kufulia," alisema.

Alisema wamechimba kisima cha maji chenye uwezo wa kutoa lita 5,000 kwa saa na kujenga mnara wenye tangi linalobeba lita 10,000 za maji.

Diwani wa Kata hiyo, Noel Shole, aliishukuru kampuni hiyo na washirika wake kwa kusaidia kuboresha sekta ya elimu katika kata yao.

"Biosustain wamefanya jambo kubwa katika kata yetu, ombi langu kwenu wananchi twendeni tukaunge mkono kampuni hii kwa kulima pamba kwa wingi katika kata yetu kwani pamba ni dhahabu," alisema.

Shole, alisema ili kufikia malengo ya kulima pamba kwa wingi, alimwagiza Ofisa Kilimo kata hiyo kuanza mikakati ya kuwahamasisha wananchi kulima pamba kwa kufanya mikutano kwa kila kijiji na kitongoji.

"Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtekente na kuagiza katika msimu huu unaoanza wa 2024/2025, shule ilime ekari tano za pamba, na mimi nitafanya ukaguzi kwa viongozi wote wa kata kuhakikisha kila mmoja amelima pamba lengo ni kuongeza uzalishaji wa zao hilo," alisema.

Alisema wananchi wanapaswa kuiunga mkono kampuni hiyo kwa kufanya upendeleo katika kata hiyo kwa kujenga bweni, jiko na kuchimba kisima cha maji.

Aliwataka wazazi ambao watoto wao watachaguliwa kwenda bwenini waache visingizio vya kuwapo na mapepo ili kuunga mkono juhudi za kampuni hiyo.

Mkuu wa Shule hiyo, Nivard Ngokotalo, alisema ujenzi wa bweni hilo utaondoa changamoto ya utoro kwa wanafunzi kutokana na kutembea umbali mrefu na kuinua kiwango chao cha elimu.

# 'Watoto nao wana msongo wa mawazo wasikilizwe'

**Na Christina Mwakangale**

OFISA Elimu Msingi, Kata ya Mikocheni, mkoani Dar es Salaam, Elizabeth Lulagora, amesema watoto nao wana msongo wa mawazo, hivyo wanahitaji kusikilizwa ili wasiingie katika matukio mabaya.

Amewataka wazazi na walezi wasiache mzigo wa malezi kwa walimu pekee kwa madai kwamba wametingwa na utafutaji fedha za mahitaji ya familia, bali nao wabebe jukumu hilo.

Elizabeth, akimwakilisha Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Kinondoni, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa mahafali ya 18 kwa wahitimu watarajiwa wa darasa la saba katika Shule ya St. Florence, Dar es Salaam.

"Mara nyingi watoto wana tabia za wale wanaoshinda nao na kuwahudumia nyumbani kama vile house girl (msichana wa kazi) au jamaa zetu.

"Watoto nao wana msongo wa mawazo, wanahitaji wasikilizwe. Mnakaa nao? Katika kata yangu, kuna mtoto alikuwa anachelewa shuleni na mwalimu mkuu wake akaamua kwenda kumtembelea.

"Kufika nyumbani, kumbe mtoto alikuwa anakwenda kuvuta bangi kwanza kisha anasubiri apate hewa harufu itoke ndipo aende shuleni.

Mwingine wa miaka 16 alimwambia mama yake 'ninataka kuacha shule niolewe', kapata mchumba!" Elizabeth alisimulia.

Alisema kuwa baada ya kupata ushauri wa mama yake, mtoto huyo alielewa na kuendelea na masomo.

"Pia kuna mambo ya ukatili wa kijinsia. Kwa miaka minne nikiwa ofisi ya kata hii, nimebaini ukatili wa kwanza huanzia ngazi ya familia," alisema.

Elizabeth pia aliwataka wazazi na walezi kuzungumza na watoto wao taaluma wanazotaka badala ya kusubiri waingie huko kwa dharura.

"Ni vizuri kuwaandaa watoto wajue na wakue katika kile wanachokipenda. Mathalani, mzazi anarudi nyumbani amelewa, anaimba watoto hawalali. Mzazi mwingine mkali na ana maneno ya kukasirisha. Hii inasababisha mtoto kupata magonjwa ya akili," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Wilson Kakamga, alisema jumla ya wanafunzi 82 ni wahitimu watarajiwa. Kati yao, wavulana ni 45 na wasichana 37.


**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**ATHUMANI JUMA BIBOZE** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE492687** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu DAR ES SALAAM tarehe 23/08/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TEM/183402/2024.**



**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 248/2024**

**Jina la Mdai: TUJIJENGE TANZANIA LTD**

**Jina la Mdaiwa: RECOCATUS LUCAS**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: REVOCATUS LUCAS**

**Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 17 Mwezi 09 Mwaka 2024 saa 5:00 asubuhi asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 Mwezi 08 Mwaka 2024.

PRIMARY COURT KINONDONI DA

HAKIMU

38

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI



**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**ELLEN KEMI MUTALEMWA** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE713220** iliyotolewa uhamiaji makao makuu tarehe 13/03/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/183526/2024.**



**KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI**

**FEDRICK ANREA NYALUKE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI TATU ZA BAJAJI ZENYE USAJILI **MC 301 BYK,MC 169 CKE, MC 307 CKD** ZILIZO POTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA KADI HIZO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/13104/2024.**



**KUPOTEA KWA CHETI**



**HANIFA IBRAHIMU GODA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S3897-0017** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Misima Mwaka 2018.Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/35745/2024**



**KUPOTEA KWA CHETI**



**HASSAN JUMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0525-0040** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MKONO WA MARA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/183586/2024.**



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 18947 OF 2024**

**In the matter of the estate of the late KRISPINA KIMARIO of Dodoma Municipal Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for Letters of administration by JOHN ESTASI MARANDU**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner thereof.

Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of SEPTEMBER ...................... 2024

Dated at Dodoma this 28 day of AUGUST................2024

RESIDENT MAGISTRATE

HABARI KIMTAIFA

# Idadi waliouawa Ukingo Magharibi yaongezeka

**JERUSALEM, Palestina**

IDADI ya watu wanaouawa katika eneo la Ukingo wa Magharibi inaongezeka wakati operesheni ya kijeshi inayofanywa na Israel ikiendelea kwa siku ya tatu.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilisema kuwa wanajeshi wake wamewaua magaidi watano wa Kipalestina, ambao wanadaiwa kujificha katika msikiti mmoja katika mji wa Tulkarm.

Juzi watu tisa waliuawa katika mashambulizi ya Israel kwenye miji kadhaa Ukingo wa Magharibi ambako Israel inaikalia kimabavu.

Kumekuwa na ongezeko la ghasia katika Ukingo wa Magharibi tangu shambulio lililofanywa na Hamas dhidi ya Israel Oktoba 7, mwaka jana na kusababisha kutokea kwa vita.

Mamia ya Wapalestina wameuawa katika eneo la Ukingo wa Magharibi tangu wakati huo, huku Israel ikisema inajaribu kukomesha mashambulizi dhidi ya Waisraeli.

Waziri mkuu wa zamani wa Israel, Ayelet Shaked, alitetea hatua za Jeshi kufanya operesheni katika Ukingo wa Magharibi akieleza ni shughuli ya kujilinda.

Shaked amekiambia kipindi cha Newsday cha BBC World Service kwamba IDF inafanya shughuli ya kuzuia mauaji mengine.

„Tuna taarifa za kijasusi kwamba Hamas inapoteza huko Gaza na wanajaribu kuwatia moyo magaidi wa Hamas katika Ukingo wa Magharibi kuanzisha mashambulizi ya kigaidi nchini Israel," alidai Shaked.

Shaked pia alikanusha madai ya maofisa wa afya wa Palestina ambao walisema kwamba jeshi la Israel limewazuia madaktari.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, ametoa wito wa kusitishwa mara moja kwa operesheni hiyo akieleza inaleta wasiwasi.

Katika ujumbe kwenye mtandao wa X, Guterres alisema kilichoondelea katika Ukingo wa Magharibi kinatia hofu.

"Nalaani vikali vifo vya watu wakiwamo watoto na naomba kusitishwa mara moja kwa oparesheni hizi," alisema.

***BBC***



Wanajeshi wa Israel wakiendelea na operesheni katika eneo la Ukingo wa Magaharibi wanakoishi Wapalestina jana. **PICHA: AFP**

# Vita vya maji Mto Nile vyanukia Misri, Ethiopia kwenye hatihati

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

ETHIOPIA imeonya kwamba kikosi kipya kinachopelekwa Somalia kupitia Umoja wa Afrika (AU), kinaweza kuzidisha hali ya mvutano zaidi katika eneo hilo la Afrika Mashariki.

Misri tayari imesema imetuma msaada wa kijeshi nchini Somalia.

Hata hivyo, Ethiopia ilielezea wasiwasi wake huo baada ya Misri ambayo kwa muda mrefu imekuwa katika msuguano na nchi hiyo kutuma vifaa vya kijeshi nchini humo.

Katika taarifa iliyotolewa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ethiopia, ilisema kwamba kanda hiyo inaingia katika hali hatari na kuongeza kuwa nchi hiyo haiwezi kukaa kimya wakati wahusika wengine wakichukuwa hatua za kuyumbisha amani ya eneo hilo.

Haikubainika wazi vifaa vya kijeshi vilivyopelekwa na Misri nchini Somalia, lakini balozi wa Somalia nchini Misri Ali Abdi, aliitaja shehena hiyo kuwa muhimu.

Abdi alisema kwamba hatua hiyo ya Misri ni ya kwanza ya kiutendaji katika kutekeleza matokeo ya mkutano wa kilele uliofanyika hivi karibuni kati ya Rais Hassan Sheikh Mahmoud na mwenzake wa Misri Abdel Fattah El-Sisi.

Kulingana na ripoti za vyombo vya habari vya Somalia, Misri itakuwa nchi ya kwanza kupeleka vikosi vyake Somalia kusaidia kuboresha usalama wa nchi hiyo baada ya kuondoka kwa kikosi cha sasa cha Umoja wa Afrika kinachojulikana kama ATMIS.

Kikosi hicho kiliundwa na nchi za Burundi, Djibouti, Ethiopia, Kenya na Uganda.

Kwa miaka mingi, Misri na Ethiopia zimekuwa katika mvutano na kurushiana maneno ya uchochezi juu ya mradi wa bwawa kubwa kwenye Mto Blue Nile, ambalo Misri inasema linatishia usalama wake wa maji.

Kwa muda mrefu, Misri imekuwa ikichukulia bwawa hilo lenye thamani ya dola bilioni 4.2 kama tishio lililopo, kwani inategemea Mto Nile kwa asilimia 97 ya mahitaji yake ya maji.

***DW***

## Wakili apinga madai dhidi mkurugenzi wa Telegram

**PARIS, Ufaransa**

WAKILI anayemtetea mmiliki wa mtandao wa kijamii wa Telegram, Pavel Durov, amesema ni udanganyifu kudai mteja wake anahusika na vitendo vya uhalifu.

Kituo cha redio cha Franceinfo na televisheni ya BFM vimeripoti jana vilimnukuu mwanasheria huyo, David-Olivier Kaminsk, akisema kuwa Telegram inafuata na kutii kikamilifu sheria za Ulaya kuhusu masuala ya kidijitali.

Kaminski , aliwaambia waandishi wa habari kuwa Telegram inasimamia sheria ambazo ni sawa na mitandao mingine ya kijamii.

Hapo jana, jaji wa Ufaransa alitaka Durov achunguzwe rasmi kwa uhalifu uliopangwa kwenye mtandao huo, lakini alimpa mwanzilishi huyo wa Telegram dhamana kwa sharti la kulipa euro milioni 5, kuripoti polisi mara mbili kwa wiki na kutoondoka Ufaransa.

Mwendesha mashtaka wa Paris, Laure Beccuau alisema katika taarifa yake kwamba jaji aligundua kulikuwa na sababu za kumchunguza Durov kutokana na mashtaka ambayo yalisababisha akamatwe siku nne zilizopita.

***DW***

## Marekani yatilia shaka ukimya wa Iran

**WASHINGTON, Marekani**

WIZARA ya Ulinzi ya Marekani, imesema kuwa kuna hatari ya Israel kushambuliwa na Iran na washirika wake.

Msemaji wa Pentagon, Meja Jenerali Patrick Ryder, aliwaambia waandishi wa habari, kuwa taarifa za umma za maofisa wa ngazi za juu wa Iran inaonesha mpango wa kuishambulia Israel bado utatekelezwa.

"Tathimini yetu ni kwamba bado kuna hatari ya kushambuliwa, na sisi bado tuko tayari kusaidia katika tukio la shambulio," alisema.

Meja Jenerali Ryder pia alisema Marekani haikuwa na jukumu lolote katika mashambulizi ya kibinadamu ya Israel au kuangusha makombora ya Hezbollah, lakini ilitoa taarifa za kijasusi kwa Israel kuhusu mashambulizi yaliyopangwa nchini Lebanon.

Msemaji huyo aliongeza kuwa waziri wa ulinzi wan chi hiyo, Lloyd Austin aliamuru makundi mawili ya wanamaji kubaki katika eneo hilo ili kuiunga mkono Israel.

Kauli hiyo ya Msemaji wa Wizara ya Ulinzi inakuja katika wakati Mkuu wa Majeshi na Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran wkusisitiza kwamba wana uhakika nchi yao itajibu mauaji ya kiongozi wa Hamas Ismail Haniyeh.

***BBC***

# Mashabiki wa Stars waitwa kushangilia

**Na Adam Fungamwango**

WINGA mpya wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Edwin Balua, amewataka mashabiki wa timu hiyo kuujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa watakapoikaribisha Ethiopia katika mechi itakayochezwa Septemba 4, mwaka huu imefahamika.

Taifa Stars imepangwa Kundi H katika mechi za kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zinazotarajiwa kufanyika mwakani nchini Morocco.

Akizungumza na gazeti hili juzi baada ya kuwasili kambini, Balua, aliyechaguliwa kutoka Simba, alisema iwapo Watanzania wataujaza uwanja, itawapa wachezaji hamasa ya kujituma na kupambana ili kupata ushindi.

Balua alisema endapo watapata ushindi katika mechi hiyo, Stars itakuwa imejiweka kwenye nafasi nzuri kuelekea kampeni hiyo ya kufuzu fainali hizo.

„Tumeanza kambi kwa ajili ya michuano hii, tuna michezo miwili, mmoja ni wa hapa nyumbani ambao tunaanza nao, ninachoomba kwa Watanzania ni wajitokeze kwa wingi kuja kutupa sapoti wakati timu yetu ya taifa itakapokuwa dimbani dhidi ya Ethiopia.

Wao wakijazana uwanjani watatupa sisi hamasa kubwa ya kupambana kwa ajili yao na taifa kwa ujumla, sisi kama wachezaji wao tunajituma kadri ya uwezo wetu ili kuwapa furaha na kulitumikia taifa," alisema Balua.

Nyota huyo pia alionyesha furaha yake ya kuchaguliwa tena kwa mara ya pili katika kikosi hicho, akisema ni heshima na faraja na akaahidi kutomwangusha Kaimu Kocha, Hemed Suleiman ‚Morocco', kwa kumteua kuwa mmoja wachezaji 23 wanaounda kikosi hicho.

"Ukipata nafasi ya kuiwakilisha nchi lazima jambo hilo ulichukulie kwa uzito, furaha yangu ni kubwa kuchaguliwa kuunda kikosi cha taifa, nchi ina wachezaji wengi hadi kuamua kunichagua mimi ni kuna kitu amekiona na naahidi kujitolea kwa asilimia 100 ili kumthibitishia mwalimu kuwa hakukosea kunichagua," winga huyo alisema.

Wachezaji wa Stars walianza kuingia kambini Jumatano iliyopita, kwa ajili ya michezo miwili ya kusaka kucheza fainali za AFCON, mmoja ukitarajiwa kupigwa Jumatano ijayo dhidi ya timu ya taifa ya Ethiopia, kabla ya kukipiga tena ugenini Septemba 10, mwaka huu dhidi ya Timu ya Taifa ya Guinea.

Stars ilishiriki fainali zilizopita za AFCON ambazo zilifanyika mapema mwaka huu nchini Ivory Coast.

# BOCCO AFUNGUKA HAJAWAHI KUTANGAZA KUSTAAFU SOKA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mkongwe nchini, John Bocco, ambaye kwa sasa ataitumikia JKT Tanzania, inayoshiriki Ligi Kuu Bara amesema hajawahi kutangaza anastaafu kucheza soka.

Kauli hiyo imekuja baada ya minong'ono ya muda mrefu ya mashabiki wa soka ambao walionyesha kushangazwa alipopewa ‚thank you' na Simba, baadaye kuonekana akiifundisha timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17, kabla ya kutangazwa kusajiliwa na JKT Tanzania.

Kwa mara ya kwanza Bocco ameibuka juzi na kujibu kuwa alipokuwa akikifundisha kikosi cha vijana cha Simba, ilikuwa ni sehemu ya mafunzo yake ya ukocha kwa vitendo kwa sababu amekuwa akisoma huku akicheza soka na wala hakuwa amestaafu.

Bocco pia alisema hata klabu yake ya zamani ya Simba haijawahi kutamka nahodha wao amestaafu, badala yake wakamwaga kwa heshima zote.

Juzi ikicheza dhidi ya Azam FC, mchezaji hiyo aliichezea JKT Tanzania kwa mara ya kwanza, ikiwa ni timu yake mpya baada ya kuitumikia Simba kwa miaka sita.

Bocco aliingia kipindi cha pili katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, na timu hizo kutoka suluhu.

"Sijawahi kusema popote kama nastaafu mpira na wala Simba haijawahi kutamka mimi nastaafu kucheza soka. Kilichotokea waliniacha kwa heshima, na mimi nikaaga, nilikwenda kuifundisha timu ya Simba chini ya miaka 17 kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo kwa kile ambacho nilikuwa nasomea," alisema Bocco.

Aliongeza aliamua kusomea ukocha mapema ili aje kuwa kocha mkubwa hapo baadaye kama ambavyo wanafanya baadhi ya wachezaji wakubwa Ulaya.

"Nimeanza kusoma mapema ili baadaye nije kuwa kocha mkubwa, niombeeni dua tu, na ndiyo malengo ya mtu yoyote anayetaka mafanikio, hata baadhi ya wachezaji Ulaya wanafanya hivyo, ila naona hapa nchini kimekuwa kitu cha ajabu kidogo," Bocco alisema.

Kuhusu kustaafu soka, alisema mpaka sasa hajafikiria hivyo, ila amebakisha misimu michache ili atundike daluga.

"Sijajua mpaka sasa nina misimu mingapi mpaka nistaafu, lakini ni michache, siyo mingi, ila kwenye timu ya taifa tayari nimemaliza.

Hapa JKT Tanzania mimi ni mchezaji, wala siyo kocha mchezaji, au kocha msaidizi," aliongeza mchezaji hiyo ambaye amewahi kuitumikia Azam FC.




Winga wa Simba Queens, Rittisia Nabbosa (kushoto), akijipanga kumtoka nyota wa Kawempe Muslim Ladies FC ya Uganda katika mechi ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Abebe Bikila ulioko Addis Ababa, Ethiopia jana. Simba Queens ililala mabao 2-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba Queens chali CECAFA

**Na Somoe Ng'itu**

SIMBA Queens imetoka patupu katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA), baada ya kufungwa mabao 2-0 na Kawempe Muslim Ladies ya Uganda kwenye mechi ya kusaka mshindi wa tatu iliyochezwa kwenye Uwanja wa Abebe Bikila jijini Addis Ababa, Ethiopia jana.

Katika mechi hiyo iliyochezwa jana asubuhi, Simba Queens ilienda mapumziko ikiwa nyuma kwa bao 1-0, na ilipoingia katika kipindi cha pili ilikubali kufungwa goli lingine ambalo liliwafanya wamalize michuano hiyo ya CECAFA wakiwa ‚kichwa chini'.

Kikosi hicho kinachoongozwa na Kocha Mkuu, Juma Mgunda, kilipoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo baada ya kufungwa mabao 2-0 na Polisi ya Kenya katika mechi ya hatua ya nusu fainali iliyochezwa mapema wiki hii.

Wawakilishi hao wa Tanzania sasa wanatarajia kurejea nchini leo kwa ajili ya kusubiri msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), ambayo itaanza baadaye mwaka huu.

Fainali ya mashindano hayo yanayosaka mwakilishi wa CECAFA katika Fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake ilitarajiwa kuchezwa jana jioni kwa kuwakutanisha wenyeji CBE dhidi ya Maafande wa Kenya.

JKT Queens ya Tanzania ndio walikuwa mabingwa wa CECAFA mwaka jana lakini walishindwa kwenda kutetea taji hilo baada ya kuvuliwa ubingwa wa hapa nchini na Simba Queens ambayo mwaka juzi ilifika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, michuano iliyofanyika Morocco.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ATLETICO YAMWINDA NUNES

KLABU ya Atletico Madrid inatathmini uwezekano wa kumsajili kwa mkopo kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes, ingawa bado hawajawasilisha ombi. ***(Athletic)***

### WARD-PROWSE ANUKIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest wanapanga kumnunua kiungo wa kati wa Uingereza, James Ward-Prowse, mwenye umri wa miaka 29, ambaye hayupo katika mipango ya kocha mpya wa West Ham, Julen Lopetegui. ***(Football Insider)***

### STERLING KUMPISHA SANCHO

CHELSEA imeonyesha nia ya kumnunua winga wa Manchester United, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, na huenda wakamjumuisha, Raheem Sterling (29), katika mkataba wa kubadilishana wachezaji. ***(Telegraph)***

### CHELSEA YAMKOMALIA OSIMHEN

CHELSEA imeanza tena mazungumzo na Napoli kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, huku masharti yakiwa mazuri zaidi kwa klabu hiyo ya England. ***(Sky Sports)***

### NKETIAH ATAKIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 25, baada ya uwezekano wake wa kwenda Nottingham Forest kutibuka. ***(Athletic)***

### WEST HAM YAMTAKA SOKER

WEST Ham inataka kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Hispania, Carlos Soler, mwenye umri wa miaka 27 kutoka Paris St-Germain lakini lazima wanalazimika kwanza wauze wachezaji wengine kabla ya kumnunua nyota huyo. ***(Guardian)***

### BARCO KUTUA SEVILLA

MLINZI wa Brighton, Valentin Barco, mwenye umri wa miaka 20 anatazamiwa kujiunga na Sevilla kwa mkopo lakini mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina haujumuishi chaguo la kumnunua. ***(Fabrizio Romano)***

### NAPOLI YAMFUATA GILMOUR

MKURUGENZI wa Napoli, Giovanni Manna, amerejea England kuendelea na mazungumzo ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Brighton na Scotland, Billy Gilmour, mwenye umri wa miaka 23, straika wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku (31), na kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay (27). ***(Gianluca di Marzio)***

### JEBBISON KIMEELEWEKA WATFORD

KLABU ya Watford imekubali mkataba wa mkopo wa msimu mzima na Bournemouth kwa ajili ya mshambuliaji, Daniel Jebbison, mwenye umri wa miaka 21, ambaye ni mzaliwa wa Canada. ***(Sky Sports)***

### WORRALL MALI YA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imekubali ombi la kumnunua mlinzi wa England, Joe Worrall, mwenye umri wa miaka 27 kutoka Burnley. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO SASA AJIPANGA KUPACHIKA MABAO 1,000

Hata hivyo Mreno huyo ashindwa kusema lini atastaafu soka...

**RIYADH, Saudi Arabia**

AKIHITAJI bao moja pekee kufikisha magoli 900 katika maisha yake ya soka kwa klabu na nchi, mfungaji bora wa muda wote, Cristiano Ronaldo, amesema anataka kufikisha mabao 1,000 ili kuacha alama yake katika mchezo huo.

Katika mahojiano na nyota wa zamani wa England, Rio Ferdinand, yaliyotolewa kwenye chaneli yake ya YouTube, Ronaldo mwenye umri wa miaka 39 alizungumza kuhusu kuweka kiwango chake cha uchezaji juu huku akiendeleza rekodi yake ya kufunga mabao.

"Nataka kufikisha mabao 1,000," alisema nyota huyo wa Al Nassr na Timu ya Taifa ya Ureno, akikadiria alama hiyo ya kihistoria inaweza kufikia akiwa na umri wa miaka 41.

Ikiwa sina majeraha yoyote, hili kwangu ndilo jambo muhimu zaidi. Nataka hilo kwangi ili kuacha alama bora ninayoweza kuwa nayo katika soka. Natakiwa kufikia magoli 900 baada ya hapo, changamoto yangu ni kuwa na mabao 1,000."

Ronaldo alizungumza kwa uwazi na Ferdinand, mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, juu ya mada kutoka kwa ubora wa uchezaji katika Ligi ya Pro ya Saudi hadi mapenzi ambayo amedumisha na ukosoaji unaotokana na hilo.

Akiwa na ushindani, Ronaldo alikuwa mwepesi kueleza malengo yake yatatofautiana na yale ya wafungaji wengine wa muda wote, wakiwamo magwiji kama vile Pele na Alfredo Di Stefano, ambao walicheza enzi ambazo kamera hazikuwa nyingi sana.

"Mabao yote niliyofunga, yana video," alisema. „Wote wana video. Sikiliza, ninawaheshimu wote Pele na Di Stefano. Na kama unataka mabao zaidi, ninaweza kuwaleta kutoka mazoezini pia. Na nitathibitisha kwa watu baadaye. Wanampendelea mchezaji huyu, au hii ndiyo bora zaidi sijali kuhusu hilo.

Alipoulizwa kuhusu kuzoea kucheza Saudi Arabia, Ronaldo alisema imekuwa rahisi kutokana na changamoto alizovumilia tangu aingie kwenye ulingo wa soka akiwa na umri mdogo.

"Hakuna nchi iliyo kamili, kwa hivyo kwangu kuzoea ilikuwa rahisi na ninapenda sana kuwa huko," alisema. „Kwa maoni yangu, ligi ni nzuri sana."

Kuhusu shutuma alizopokea kwa kulia baada ya kukosa penalti muhimu dhidi ya Slovenia na safari ya robo fainali ya Euro 2024, Ronaldo alisema yote hayo ni sehemu ya uchunguzi unaokuja na kuwa "mtu anayefuatiliwa zaidi duniani." Ureno walishinda mechi hiyo kwa mikwaju 3-0.

Machozi hayo alisema ni matokeo ya shinikizo alilojiwekea tangu akiwa na umri wa miaka 11.

"Unapokuwa na shauku kwa kile unachofanya, huwezi kuwa na wasiwasi kuhusu jinsi unavyohisi," alisema.

"Nilishindwa kwa sababu nilijiwekea presha tangu nikiwa na umri wa miaka 11. ‚Cristiano, wewe ni mchezaji bora zaidi duniani,' huwa nawaza hivyo.

"Lakini nilipokosa penalti, nilijisikia vibaya kwangu, mashabiki, familia, sio kwa sababu ya mambo mengine ambayo watu wanasema."

Ingawa anatambua anakaribia mwisho wa uchezaji wake mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or hakutabiri ni lini atatundiga daruga.

"Sijui nitamaliza lini," alisema. "Kwa kuwa unacheza zaidi, unajifunza vitu vingi sana. Jambo moja ambalo nimejifunza ni kufurahia wakati huo. Kwa sababu hujui kitakachotokea kesho. Najua bado ninaonekana mzuri. Siku ambayo ninaanza kuhisi sizalishi chochote, sikiliza, nitapakia virago vyangu na nitaondoka."

# CHIESA ATUA RASMI LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imekamilisha mchakato wa kumsajili, Federico Chiesa, baada ya kufikia makubaliano ya ada ya uhamisho na Juventus.

Mshambuliaji huyo mwenye uwezo mkubwa tayari amesafiri kwenda England kukamilisha uchunguzi wa afya na kukamilisha taratibu za mwisho zilizosalia za mkataba huo.

Fabrizio Romano ameripoti Liverpool na imekubali kulipa euro milioni 13 ya awali pamoja na nyongeza.

Juventus ilikuwa ikitafuta kurejesha euro milioni 15 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia, ambaye hakuwa sehemu ya mipango ya Kocha Mkuu, Thiago Motta.

Baada ya kumsajili kutoka Fiorentina mnamo 2020 kwa euro milioni 50, Juventus inaweza kupata hasara kubwa kwa Chiesa, ambaye anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka minne na Liverpool.

Kabla ya safari yake ya ndege kutoka Italia kwenda England, Chiesa aliliambia Gazzetta dello Sport: "Nina furaha sana na niko tayari kwa tukio hili jipya, ningependa kutuma salamu kwa mashabiki wa Juventus."

The Athletic liliongeza Chiesa amekuwa akilengwa kwa muda mrefu na Liverpool, na kwa kuwa alipatikana kwa bei iliyopunguzwa, klabu hiyo ilihamia 'kuboresha hali'.

Baada ya kuwasiliana na Juve kwa mara ya kwanza Jumatatu, Wekundu hao wamechukua hatua haraka kufikia makubaliano huku kulikuwa na ofa kutoka Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye ana uwezo wa kucheza popote kwenye mstari wa mbele, anaondoka Juventus akiwa amefunga mabao 32 katika mechi 131.

Chiesa aliunda sehemu muhimu ya timu ya Italia iliyoshinda Euro 2020, wakati pia alikuwa kwenye kikosi chao kilichoshindwa kutetea taji kwenye Euro 2024 mapema msimu wa joto.




## Arsenal yamuuza Ramsdale

**LONDON,** England

ARSENAL imefikia makubaliano kumuuza Aaron Ramsdale, katika klabu ya Southampton kwa mkataba wa mwaka mmoja baada ya kuamua kumweka benchi na nafasi yake kupewa, David Raya.

Ramsdale aliteuliwa katika Timu Bora ya PFA ya msimu wa mwaka 2022/2023 Washikabunduki walipotoa ushindani mkubwa wa kuwania taji la kwanza la Ligi Kuu katika miaka 15.

Lakini mambo yalibadilika haraka sana wakati Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alipoamua Raya angefaa zaidi kimbinu. Mhispania huyo aliwasili kutoka Brentford kwa mkopo na amepewa mkataba wa kudumu.

Hata hivyo, Ramsdale anaonekana kuweka kazi yake kwenye mstari. Gazeti la Athletic limeripoti Arsenal wamekubali uhamisho wa pauni milioni 25 ambao unajumuisha nyongeza.




Uchunguzi wa kimatibabu ni hatua inayofuata, lakini kila kitu kinaelekeza ajiunge na Watakatifu kabla ya siku ya mwisho ya usajili ambayo ni leo.

Kwa upande wake, Arsenal "itaendeleza juhudi zao" kumsajili Joan Garcia kutoka Espanyol kama mbadala.

Kwa Ramsdale, inamaanisha amerudi katika Pwani ya Kusini. Kipa huyo mzaliwa wa Stoke alijiunga na Bournemouth kwa pauni 800,000 kutoka Sheffield United akiwa na umri wa miaka 19 na akatumia miaka mitatu na nusu akiwa na Cherries hao.

Alikuwa mwanzilishi katika msimu wake wa mwisho huko 2019/20, kabla ya kurejea Sheffield kwa pauni milioni 18.5.

Mwaka mmoja baada ya hapo, Arsenal walikubali mkataba wa pauni milioni 24 kumsajili.

Kipa mkongwe, Alex McCarthy, amerejeshwa kama namba moja wa Southampton hadi sasa msimu huu, huku Gavin Bazunu akikosa kucheza kwa muda mrefu kutokana na jeraha la mguu.

## Nunez afungiwa mechi tano

**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Darwin Núñez, atatumikia adhabu ya kutocheza mechi tano za kimataifa kama sehemu ya adhabu iliyotolewa na Shirikisho la Amerika Kusini (CONMEBOL), kutokana na matukio ya nusu fainali ya Uruguay ya Copa América dhidi ya Colombia mwezi uliopita.

Nuñez, mmoja wa wachezaji watano wa Uruguay watakaofungiwa, sasa atakosa mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la 2026 dhidi ya Paraguay, Venezuela, Peru na Ecuador. Pia, alipigwa faini ya Dola za Marekani 20,000.

Michezo ya ndani haijajumuishwa katika adhabu hiyo kwa hivyo ushiriki wa Nuñez na Liverpool hautaathiriwa.

Kiungo wa Tottenham Hotspur, Rodrigo Bentancur, naye amefungiwa michezo minne na kutozwa faini ya Dola za Marekani 16,000, huku José María Giménez, Mathías Olivera na Ronald Araújo kila mmoja akifungiwa michezo mitatu na faini ya Dola 12,000.

Kufuatia ushindi wa 1-0 wa Colombia mjini Charlotte, North Carolina, Julai 10, wachezaji na wafanyakazi kadhaa wa Uruguay walipanda viwanjani kukabiliana na mashabiki, huku CONMEBOL ikianzisha uchunguzi kuhusu suala hilo siku iliyofuata.

Wachezaji walionekana wakijihusisha na vurugu za kimwili na mashabiki wa Colombia kwenye Uwanja wa Bank of America, na video baadaye zikitokea za Núñez alionekana akijaribu kutupa kiti kwenye umati.

Wachezaji sita ambao hawakuhusika katika tukio hilo, walipokea faini ya dola 5,000 ambapo ni Matías Viña, Sebastián Cáceres, Brian Rodríguez, Emiliano Martinez, Santiago Mele na Facundo Pellistri.

Shirikisho la Soka la Uruguay kwa ujumla lilitozwa faini ya dola 20,000, huku Ofisa wa shirika hilo, Marcelo Garcia, akipigwa marufuku kushiriki mashindano yote ya CONMEBOL kwa miezi sita baada ya kuonekana akiwarushia chupa ya maji mashabiki kutoka kwenye chumba chake kwenye Uwanja wa Bank of America.

Kocha Mkuu, Marcelo Bielsa, alitetea kitendo cha timu yake wakati huo, akisisitiza wachezaji walikuwa wanajilinda tu na kujaribu kuwalinda wanafamilia.

"Kitu pekee ninachoweza kukwambia ni wachezaji waliitikia kama binadamu mwingine yeyote," alisema.

"Ukiona kuna mchakato wa kuzuia kilichotokea kisifanyike. Ukiona ikiwa kile kilichotokea kitatokea, na eti kuna mchakato mwingine - njia ya kutoroka, tuseme - na mambo yote mawili hayatafanikiwa."



HABARI MICHEZO

# NYAMBAYA AULA TENA DRFA, NYAMLANI AKEMEA MIGOGORO

**Na Mwandishi Wetu**

LAMECK Nyambaya amechaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), kwa kupata kura zote 11 katika uchaguzi uliofanyika kwenye Ukumbi wa King Jada jijini jana.

Mkutano huo wa uchaguzi pia ulimuidhinisha Benny Kisaka kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho huku Juma Pinto akichaguliwa kwa kura zote kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Kondo Mussa aliyepata kura 10 na Ramadhani Shauritanga (kura sita), walichaguliwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya DRFA wakati Chichi Mwidege alitangazwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa kuteuliwa.

Mjumbe mwingine wa Kamati ya Utendaji aliyetangazwa jana ni Somoe Ng'itu ambaye anaingia moja kwa moja kwa sababu ni Mwenyekiti cha Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Dar es Salaam (DWFA).

Akifungua mkutano huo wa uchaguzi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani, aliwataka wajumbe wa mkutano huo kujiepusha na migogoro na badala yake kuwekeza nguvu katika kuhakikisha soka linachezwa kwa ubora wa juu hapa jijini.

Nyamlani alisema Dar es Salaam ndio kioo cha soka hapa Tanzania, hivyo anataka kuona ushindani wa ligi zake unarejea kama ilivyokuwa miaka ya nyuma pamoja na kuzalisha waamuzi, makocha na wachezaji mbalimbali.

"Kioo cha mazingira ya mpira wetu ni Dar es Salaam, kuna mahala fulani tulipotea, Dar kukawa hakuna tena ile hadhi yetu hadi ikaondolewa kutoka Kanda na kuwa mkoa kama Katavi au Lindi, hii hapana, tufanye mabadiliko, turudi kule tulipokuwa," Nyamlani alisema.

Aliongeza anataka kuona vyama vya wilaya za Dar es Salaam vinakuwa imara na si sehemu ya 'magenge' ya watu kujitafutia maslahi binafsi.

"Hatutaki migogoro, tunataka katiba mpya, katiba imara, wacheni tuifufue Dar es Salaam, tuweke maslahi binafsi pembeni, matendo yafanane na mkoa wa Dar es Salaam, tutengeneze waamuzi, tuhakikishe waamuzi bora watoke hapa, wenzetu wanampango ndio maana wamefanikiwa kuzalisha waamuzi bora, tuzalishe makocha, tuwe kitovu cha kila kitu cha mpira wa Tanzania," Nyamlani aliongeza.

Baada ya kutangazwa mshindi, Nyambaya aliwashukuru wajumbe wa mkutano mkuu na kuahidi kuinyanyua upya Dar es Salaam ili iwe tishio kama ilivyokuwa miaka iliyopita.

## JKT yafurahia kuibana Azam

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kugawana pointi, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, amewapongeza wachezaji wake kwa kuonesha kiwango kizuri katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC.

JKT Tanzania ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Isamuhyo ilifanikiwa kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Azam FC ambayo iliingia katika mechi hiyo ikiwa pia na machungu ya kuondolewa kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili, Ally, alisema licha ya kutarajia kupata ushindi katika mchezo huo wa nyumbani, anawapongeza wachezaji wake kwa kufuata vyema maelekezo aliyowapa.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wamefanya kile alichowaelekeza walipokuwa ndani na nje ya uwanja kuelekea mechi hiyo.

"Ninawapongeza wachezaji wangu kwa uwezo walioonyesha katika mchezo huu tukiwa nyumbani, haikuwa mechi rahisi kwa kila upande," alisema kocha huyo.

Aliongeza anafahamu ligi ni ngumu, hivyo amewaandaa wachezaji wake kucheza soka la ushindani katika kila mechi iliyoko mbele yao.

"Tumemaliza mechi hii, sasa akili yetu na mipango ni kuelekea mchezo ujao, ninarudia tena hakuna mechi rahisi, naendelea kuwapongeza wachezaji na kuwashukuru mashabiki wetu kwa ushirikiano," Ally alisema.

Aliongeza lengo lake ni kufanya vizuri katika kila mchezo ili kufikia malengo ya kumaliza msimu kwenye nafasi tano za juu.




Kiungo wa Azam FC, Iddi Suleiman 'Nado' (kushoto), akijipanga kumtoka kiungo wa JKT Tanzania, Saidi Ndemla katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Isamuhyo, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: MTANDAO**

## Waamuzi waaswa kuzingatia weledi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAAMUZI wa soka nchini wametakiwa kufanya kazi kwa weledi na malengo ili kupiga hatua na kupata nafasi ya kuchezesha mechi za kimataifa, imeelezwa.

Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Suleiman Mahmoud Jabir, alisema hayo juzi wakati akifunga mafunzo ya siku nne kwa waamuzi wa mchezo huo visiwani hapa.

Jabir alisema fani hiyo ni muhimu na ni 'fani mama' katika ustawi wa soka hivyo lazima waamuzi wajitengenezee njia nzuri zitakazowafanya kupata michezo ya kimataifa.

"Uamuzi ni kazi ngumu na hakuna jambo ambalo utalifanya likaonekana kuwaridhisha watu, cha msingi ni kutimiza wajibu wako na kufanya kazi ili usiwe katika chanzo cha matatizo," alisema Jabir.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi Zanzibar, Waziri Sheha, alisema mafunzo hayo ambayo yalianzia Pemba na kumalizika Ugunja yalishirikisha waamuzi 66 na kati ya hao wanawake walikuwa 10.

## Netiboli Daraja la 2 kufanyika Kilimanjaro

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya Netiboli Daraja la Pili imepangwa kufanyika kuanzia Oktoba 19 hadi 29, mwaka huu katika Mji wa Moshi mkoani, Kilimanjaro.

Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Hilda Mwakatobe, alisema jana mpaka tayari wamezitumia taarifa timu 13 ambazo zinatakiwa kushiriki mashindano hayo.

Mwakatobe alisema maandalizi ya ligi hiyo yanaendelea vyema na kuzitaka timu kuthibitisha ushiriki wao kabla ya Septemba 20, mwaka huu.


"Tunatarajia mashindano haya yatakuwa na upinzani mkubwa kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri, tunawaomba waendelee na maandalizi kwa sababu hakutakuwa na mechi rahisi," alisema Mwakatobe.

Aliongeza chama hicho kinaziomba taasisi na kampuni mbalimbali kujitokeza kuwaunga mkono ili kufanikisha ligi hiyo ambayo itasaidia kupata wachezaji watakaojiunga na timu za taifa.

Michezo
Ijumaa Agosti 30, 2024
Nipashe

Ronaldo sasa ajipanga kupachika mabao 1,000

UKURASA 21






Straika wa kimataifa wa Yanga, Prince Dube (kulia), akifanya shambulizi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera jana. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yatoa dozi Kagera

## Yaweka rekodi kutofungwa mechi ya ufunguzi katika misimu 10 mfululizo...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO yaliyofungwa na Mkongomani Maxi Nzengeli na straika, Clement Mzize yaliwapa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, mchezo uliochezwa Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba, Kagera jana.

Ulikuwa ni mchezo wa raundi ya kwanza kwa Yanga ambayo ilikuwa katika mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, huku ulikuwa ni mchezo wa pili kwa Kagera Sugar.

Ushindi huo umeifanya Yanga kutopoteza kupoteza mechi ya raundi ya kwanza kwa misimu 10 mfululizo tangu msimu wa mwaka 2014/2015.

Mara ya mwisho Yanga kupoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni Septemba 20, 2014 ilipofungwa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro dhidi ya Mtibwa Sugar, mabao yaliyofungwa na Mussa Hassan ‚Mgosi' na Ame Ally.

Kama wachezaji wa Yanga wangekuwa makini wangeweza kwenda mapumziko wakiwa na mabao sita, huku Dube peke yake akikosa magoli manne ya wazi.

Sifa kubwa ziende kwa golikipa wa Kagera Sugar, Ramadhani Chalamanda, ambaye alikuwa shujaa wa kupunguza idadi ya mabao ya kufungwa, kwa sababu alifanikiwa kudaka na kupangua michomo ya hatari kutoka kwa wachezaji wa Yanga waliokuwa na ‚uchu'.

Dakika ya kwanza tu, tayari Yanga walianza kulisabahi lango la Kagera Sugar, ambapo Stephane Aziz Ki, alimpenyezea Dube aliyekuwa katika nafasi nzuri kabisa, lakini shuti lake lilikamatwa na kipa Chalamanda kwa ustadi mkubwa.

Aziz Ki naye alikosa bao dakika ya saba, baada ya makosa ya mabeki wa Kagera Sugar, alijikuta akibaki wa kipa, lakini shuti lake lilikuwa dhaifu ambalo halikumpa tabu.

Kwa mara nyingine tena, Dube alikosa bao dakika ya 18, baada ya wachezaji Aziz Ki, Mudathir Yahaya na Nzengeli kugongeana, mpira ukamkuta Pacome Zouzoua, ambaye aliurudisha nyuma kidogo kwa pasi ya kisigino, iliyomkuta Mzimbabwe huyo aliyepiga shuti mpira ukapanguliwa na kipa.

Dakika ya 21, pasi nyingine ya Aziz Ki, ilimkuta Dube, lakini alishindwa kuupachika mpira wavuni.

Hata hivyo, dakika tatu baadaye Nzengeli aliwafundisha wenzake jinsi ya kuuweka mpira ndani ya wavu, alipopachika bao maridadi kwa shuti kali la mguu wa kulia.

Bao hilo bado halikufanya Yanga waendelee kukosa mabao ya wazi kwani dakika ya 31, Dube aliendelea kukosa mabao, na dakika ya 39 ilikuwa ni zamu ya Pacome, huku Chalamanda akiendelea kuwa shujaa.

Mpaka timu zinakwenda mapumziko, hakukuwa na shambulizi lolote la maana kwa Kagera Sugar zaidi kona mbili ambazo hazikuzaa matunda, lakini angalau kipindi cha pili, mabeki wa Kagera Sugar walionekana kupunguza makosa.

Pia Kagera Sugar ilifanikiwa kufanya mashambulizi mawili ya nguvu dakika ya 52 na 59 ambayo kama wachezaji wake wangeweza kupata mabao, krosi iliyopigwa na Joseph Mahundi ilimkuta straika Peter Lwasa, lakini akipiga kichwa dhaifu akiwa hajakabwa, mpira ukatoka nje.

Dakika saba baadaye, kipa Djigui Diarra alifanya kazi ya ziada kuchupa na kuidokoa krosi ya Geofrey Manyasi ambayo ilikuwa inasuburiwa na Judica Mafie ili aukwamishe wavuni, hivyo kukwamisha malengo yake.

Mzize alifunga bao la pili dakika mbili kabla ya mechi kumalizika, aliunganisha krosi ya Aziz Ki.

Kwa matokeo hayo Yanga ina pointi tatu na mabao mawili, huku Kagera Sugar iliyocheza mechi mbili ikiwa haina pointi wala bao, ikiruhusu mabao matatu.

## Simba yafunguka, Dabo hana presha

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI uongozi wa Simba ukisema umeamua kuandaa mechi ya kirafiki ili kuendeleza ‚joto' kwa wachezaji wake, Kocha wa Azam FC, Yousouph Dabo, amesema hana presha wala hofu ya kutimuliwa kufuatia matokeo mabaya ambayo timu yake imepata.

Simba inatarajia kukutana na Al Hilal ya Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam ili wachezaji wake wasikae muda mrefu bila kucheza na kujirudia kilichowapata wakati wanaivaa UD Songo ya Msumbiji pamoja na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini mwaka juzi.

Simba inatumia mechi ya kesho kujiandaa kuwakabili Al Ahly Tripoli ya Libya katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaopigwa ugenini Septemba 13, mwaka huu huku marudiano yakifanyika baada ya wiki moja hapa nchini.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamejifunza mengi katika michezo kadhaa ya kimataifa ambayo walikaa muda mrefu bila kucheza ambayo ilipelekea wachezaji wao wasiwe na utimamu mzuri wa mwili.

„Tuna sababu tatu za kiufundi kwa nini tumeileta Al Hilal tucheze mchezo huu wa kimataifa ya kirafiki. „Kumbuka tumecheza mchezo wa mwisho tarehe 26, na mchezo unaofuata ni wa kimataifa ambao utacheza Septemba 13, hapo ni kiasi cha siku kama 17 hivi, haiwezekani tukae siku zote hizi, hii imeshawahi kutuumiza huko nyuma," alisema Ahmed.

Aliongeza wachezaji wa Simba hawawezi kukaa siku zote hizo bila kucheza hasa ikizingatiwa baadhi ni wapya, wanahitaji kuendelea kuzoeana.

„Kwanza kabisa wachezaji wetu walishaanza kupata muunganiko, na mwendo, wakikaa siku zote hizo, utimamu wa mwili utashuka, kila kitu kitapotea na timu inaweza hata kupoteza mechi," aliongeza Ahmed.

Wakati huo huo, ikiwa zimepita siku chache wameondolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutoka suluhu dhidi ya JKT Tanzania juzi, Dabo aliliambia gazeti hili hana presha yoyote na kazi yake.

Dabo alisema matokeo hayo si mazuri kwao lakini ndivyo mpira ulivyo.

„Nilikuwa kocha hata kabla sijaja Azam na nitaendelea kuwa kocha, sina presha yoyote kwa sababu sifanyi kazi kwa presha, matokeo si mazuri, tulitarajia ushindi lakini imeshindikana. Tutarejea na nguvu mpya katika mchezo ujao," alisema Dabo.

**Imeandaliwa na Faustine Feliciane na Adam Fungamwango.**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >